OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

TOLEO MAALUM LA MWANANCHI LA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

www.nao.go.tz

" Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za mwananchi "

Ibara ya 18 (2)

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jengo la Ukaguzi, Mtaa wa Hazina, S.L.P 950, 41104 Dodoma, TANZANIA
Simu:+255 (26) 2321759, Nukushi: +255 (26) 2321245
Barua pepe: ocag@nao.go.tz | Tovuti: www.nao.go.tz

TOLEO MAALUM LA MWANANCHI LA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI (CAG) KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

YALIYOMO

YALIYOMO ii

UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.................... 1

DIBAJI 5

SURA YA KWANZA 8

1.0 UTANGULIZI 8

SURA YA PILI 13

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI NA HATI ZA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA 13

SURA YA TATU 17

3.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.. 17

SURA YA NNE 20

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2017/18 20

SURA YA TANO 29

5.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 29

SURA YA SITA.. 42
6.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA......................... 42

SURA YA SABA.. 52
7.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO....................... 52

SURA YA NANE.. 60
8.0 RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI.. 60

SURA YA TISA.. 75
9.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) 75

" Taarifa hizi zinalenga kuongeza chachu ya uwajibikaji wa makundi mbalimbali yenye dhamana ya kusimamia rasilimali za Umma. "

Charles E. Kichere

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

UJUMBE WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ibara ya 143 (2) (C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (pamoja na mrekebisho yake), inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha zilizoandaliwa na Maafisa Masuuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taarifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha za Bunge na kutoa taarifa ya ukaguzi angalau mara moja kila mwaka.

Ninayo furaha kutambulisha kitabu cha sita (6) cha Toleo Maalum kwa Mwananchi kuhusu Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Upashanaji habari miongoni mwa jamii ni kati ya masuala muhimu yaliyoainishwa katika Ibara ya 18 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inasema; “Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za mwananchi”

Toleo la mwaka huu 2019 ni la sita ambapo toleo la kwanza lilitolewa mwaka 2012. Toleo hili linahusu hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2018, pamoja na taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2019. Katika toleo hili msomaji atapata matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa Serikali Kuu; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mashirika ya Umma; na Miradi ya Maendeleo.

Aidha, toleo hili linajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Pia, taarifa hii inawasilisha Ripoti 11 za Ukaguzi wa Ufanisi katika sekta mbalimbali ambazo ni:

a) Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji;
b) Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini;
c) Usimamizi wa Miradi ya Maji ya Visima Virefu;
d) Matengenezo ya Mitambo ya Kuzalisha Umeme;
e) Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum;
f) Usimamizi wa Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa pamoja;
g) Ufuatiliaji wa Shughuli za Ujenzi wa Majengo Mijini;
h) Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura kwa Hospitali za Rufaa ngazi ya Juu;
i) Upatikanaji na Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo;
j) Usimamizi wa Utoaji wa Huduma ya Bima ya Taifa ya Afya Nchini; na
k) Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi.

Toleo hili linaandaliwa kwa lugha rahisi na nyepesi, lengo likiwa ni kuongeza uelewa kwa jamii juu ya ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za umma. Taarifa hizi zinalenga kuongeza chachu ya uwajibikaji wa makundi mbalimbali yenye dhamana ya kusimamia rasilimali za Umma.

Ninapenda kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake na kufanikisha maandalizi ya toleo hili. Aidha, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kazi kubwa waliyofanya ili kuhakikisha toleo hili linapatikana kwa wakati.

Ninawahimiza wananchi wote kukisoma kitabu hiki kwani watafahamu kwa kina kazi zinazofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pamoja na taarifa za ukaguzi zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais tarehe 28 Machi, 2019.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali **Novemba, 2019**


WANANCHI WANARUHUSIWA KUFUATILIA TAARIFA ZA UKAGUZI WA TAASISI ZA UMMA?
SHERIA YA FEDHA INAZITAKA WIZARA, WAKALA NA IDARA ZA SERIKALI KUHAKIKISHA WANATOA TAARIFA ZA SHUGHULI NA RASILIMALI ZA TAASISI ZA UMMA.

DIBAJI

Toleo hili kwa ajili ya wananchi limegawanyika katika sehemu kuu tisa. Taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 June 2018 pamoja na ukaguzi wa Ufanisi na ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Sura ya Kwanza: Sura hii inatoa maelezo ya utangulizi wa kitabu hiki, wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, madaraka yake, dhima na dira ya ofisi, misingi ya uadilifu pamoja na ufafanuzi wa baadhi ya maneno yaliyotumika katika kitabu hiki.

Sura ya Pili: Sura hii inatoa maelezo kuhusu kaguzi mbalimbali, aina na tafsiri ya hati, idadi ya hati za ukaguzi zilizotolewa kwa kaguzi za Serikali Kuu, Serekali za Mitaa,Mashirika ya Umma na Miradi ya Maendeleo,Ufanisi, ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Kaguzi Maalum kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2018.

Sura ya Tatu: Sura hii inaonesha utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za kipindi kilichopita katika ukaguzi wa hesabu za Serikali.

Sura ya nne: Sura hii inatoa muhtasari wa Ukaguzi wa Serikali Kuu yenye mafungu 65 ambayo yanajumuisha Wizara na Taasisi; Sekretarieti za Mikoa 26; Wakala wa Serikali 33; Mifuko Maalum 16; Ofisi za Balozi za Tanzania 41; Bodi na Mamlaka za Maji 14; taasisi nyinginezo 42; Mifuko Jumuifu 2; Mamlaka ya Mapato Tanzania na Vyama vya Siasa14.

Sura ya Tano: Sura hii inaonesha muhtasari wa ukaguzi wa hesabu za Serikali za Mitaa (Halmashauri) 185 zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha 2017/18.

Sura ya Sita: Sura hii inahusu muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018.

Sura ya Saba: Sura hii inaonesha muhtasari wa kaguzi za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Miradi ya maendeleo inajumuisha miradi mikubwa minne inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wahisani kupitia mfuko wa pamoja. Miradi minne ya maendeleo ambayo huchangiwa kwa pamoja na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Afya (HBF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Programu ya Maendeleo Sekta ya Maji (WSDP). Aidha, ukaguzi umefanyika katika miradi mingine inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa (UN) na wadau wengine wa maendeleo.

Sura ya nane: Sura hii inatoa Muhtasari wa kaguzi kumi na moja (11) za Ufanisi zilizofanyika kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2019. Ukaguzi wa ufanisi hubainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali ikiwemo malalamiko kutoka kwa wananchi, umuhimu wa eneo husika kiuchumi na kijamii kwa kutumia vigezo vilivyowekwa na ofisi. Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni; Miradi ya Maji vijijini, Ujenzi wa Majengo vijijini, ukaguzi wa Visima virefu vya maji, Ukaguzi wa Uzalishaji Umeme,Ukaguzi wa Wanafunzi Wenye mahitaji Maalum,ukaguzi wa Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Bima ya Afya zinazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Taarifa ya Ufanisi ya Upatikanaji na Usambazaji wa Pembejeo Bora za Kilimo

Sura yaTisa. Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa TEHAMA hasa mifumo mikubwa mitatu (3). Mifumo hiyo ni; Mfumo wa Hesabu wa Serikali za Mitaa (IFMS Epicor) katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu serikalini (Lawson) katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki (GePG) katika Wizara ya Fedha na Mipango. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inakaribisha Maoni ili kuboresha toleo la kitabu hiki maalum kwa ajili ya wananchi katika toleo lijalo.


MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA
NIPISHE!
HUDHANI KWAMBA KUNA UMUHIMU WA KUIMARISHA UDHIBITI WA MATUMIZI YAKO ILI RASILIMALI ZA UMMA ZITUMIWE KAMA ZILIVYOKUSUDIWA?

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Madaraka, Majukumu na Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Pamoja na marekebisho yake) pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

1.1 Wajibu na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 136 (3); matumizi yote kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali, yatafanyika mara tu baada ya kuidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

1.2 Madaraka

Baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha Ripoti yake kwa Rais, ripoti hiyo itawasilishwa katika kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika mara baada ya Rais kupokea Ripoti. Kwa mujibu wa kanuni ya 8(5) ya kanuni ya sheria ya fedha za Mwaka 2001(iliyorekebishwa 2004), kila Wizara, Wakala na Idara za Serikali inajukumu la kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu shughuli za fedha za taasisi zinatolewa kwa umma. Hivyo basi taasisi hizo zinapaswa kuandaa na kuhakikisha kuwa umma unapata taarifa za mwaka za bajeti, malengo na mipango ya kila program, tathmini ya utekelezaji wa malengo, muhtasari wa matokeo ya taarifa za fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa Ripoti kila Mwaka, wananchi wa kawaida huwa ni vigumu kupata Ripoti hizo kwa wakati. Ofisi iliamua kwa mara

ya kwanza Mwaka, 2012 kutoa Toleo Maalum kwa ajili ya wananchi. Kitabu hiki humwezesha mwananchi yoyote kupata ujumbe uliomo katika taarifa za ukaguzi kwa sababu lugha iliyotumika ni pamoja na picha (vibonzo).

Napenda kusisitiza kuwa wananchi wana haki ya Kikatiba na Kisheria ya kupata taarifa sahihi zinazohusu uendeshaji wa taasisi mbalimbali za umma. Hivyo ni wajibu kwa kila mwananchi kudai taarifa zilizotajwa hapo juu ili kuweza kufanya tathimini ya Utendaji wa taasisi hizo.

1.3 Dira: Kuwa Taasisi ya Kiwango cha Juu katika Ukaguzi wa Sekta ya Umma.

1.4 Dhima: Kutoa Huduma za Ukaguzi wa Sekta ya Umma Zenye Ubora wa hali ya Juu zinazoimarisha Utendaji, Uwajibikaji na Uwazi Katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

1.5 Misingi ya Uadilifu

Kutopendelea: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki pasipo upendeleo.

Ubora: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa kitaalam.

Uadilifu: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu Sheria.

Zingatio Kwa Wadau: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inalenga matakwa ya wadau Kwa kujenga utamaduni wa kutoa huduma bora Kwa wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na ari ya kazi.

Ubunifu: Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi inayothamini ubunifu wakati wote, inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya Taasisi

1.6 Haki ya Mwananchi Kupata Taarifa

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka bayana kuwa, taarifa ni haki ya mwananchi. Aidha, Sheria Na. 6 ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016 na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 zimeweka utaratibu wa utoaji taarifa kwa misingi ya sheria. Ofisi hutoa Toleo Maalum kwa ajili ya wananchi ili waweze kupata Taarifa za kikaguzi.

Taarifa za Ukaguzi Kwa mujibu wa kanuni ya 8 (5) ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004); Wizara, Wakala na Idara za Serikali zina jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa kuhusu shughuli na rasilimali za taasisi husika zinatolewa kwa umma. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuandaa taarifa za mapato na matumizi yake kisha kila mwananchi kutafuta taarifa hizo ili kufuatilia utekelezaji wa shughuli za maendeleo nchini.

1.7 Rasilimali za Taifa na Uwajibikaji

Rasilimali za Taifa zinajumuisha fedha, maliasili ya nchi,watu, ardhi na mambo mengine yote yanayohitajika katika uendeshwaji wa Serikali kama ilivyoelezwa katika ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977

(pamoja na mrekebisho yake). Kwa mujibu wa muundo, mipaka na mamlaka katika usimamizi wa rasilimali za Taifa kati ya mihimili mitatu ni kama ifuatavyo:

1.7.1 Bunge

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi lina wajibu wa kuidhinisha na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali. Wananchi kupitia wabunge wao wanaweza kutoa maoni yao ya namna ambavyo wangependa Serikali iweze kutatua matatizo yao.

1.7.2 Serikali

Serikali inawajibu wa kukusanya na kutumia rasilimali za Taifa kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Serikali imegawanyika katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika na Taasisi za Umma.

1.7.3 Mahakama

Mahakama wana wajibu wa kusikiliza mashauri yote yanayofikishwa Mahakamani na kutoa hukumu kulingana na sheria za nchi.

UMETUAIBISHA MBELE YA MGENI RASMI, ULISEMA CHINI KUNA MAJI, TUKACHIMBA KISIMA CHA MILIONI MIA SABA, HOLA! HAMNA MAJI!!!
LAKINI MIE NILIPOPIMA CHINI NILIONA UNYEVU NYEVU...

SURA YA PILI

2.0 MAELEZO YA JUMLA KUHUSU UKAGUZI NA HATI ZA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kukagua na kutoa maoni ya ukaguzi kwa mkaguliwa juu ya hesabu zilizoandaliwa na kazi zilizotekelezwa. Maoni ya ukaguzi yanayotolewa ni maelezo mafupi kuhusu kiwango cha usahihi kilichofikiwa katika utayarishaji wa taarifa za fedha na uzingatiaji wa sheria mbalimbali zinazogusa shughuli za kila siku za uendeshaji Taasisi za Umma, Wizara, Mashirika ya Umma na mamlaka za Serikali za Mitaa.

2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo hutolewa baada ya ukaguzi kukamilika. Kila hati inaelezea mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Aina hizo ni kama ifuatavyo: **Hati inayoridhisha, Hati yenye shaka, Hati isiyoridhisha na Hati mbaya.**

2.1.1 Hati inayoridhisha

Hati hii hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa zinakuwa zimezingatia matakwa na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya Umma ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa sheria na kanuni.

2.1.2 Hati yenye shaka

Hati yenye shaka hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhasibu ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa sheria na kanuni lakini

bado mkaguzi anaona kuna mapungufu yaliyojitokeza ambayo kwa ujumla yanatakiwa kufanyiwa kazi. Mfano ni pale ambapo mkaguzi hakupewa vielelezo na ushahidi wa kutosha lakini amejiridhisha kwamba athari ya kukosekana kwa vielelezo hivyo sio kubwa kwenye hesabu zilizokaguliwa. Kwa hiyo, hati itaonyesha kuwa hesabu kwa ujumla zimeandaliwa vizuri isipokuwa kasoro chache zilizohojiwa.

2.1.3 Hati isiyoridhisha

Hati hii hutolewa wakati inapogundulika kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa kwa kiasi kikubwa zina kasoro kwa sababu kwa ujumla wake hazikuandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya uhasibu katika sekta ya umma ikiwa ni pamoja na uzingatiaji wa sheria na kanuni. Maelezo ya maeneo yenye mapungufu huainishwa ili kumsaidia mkaguliwa kuelewa sababu zilizopelekea kupata hati isiyoridhisha.

2.1.4 Hati mbaya

Hati hii hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa hazina vielelezo vya kutosha hali hii husababisha kuwepo kwa ufinyu mkubwa sana wa mawanda ya ukaguzi. Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wowote kuhusu hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo humfanya mkaguzi kwa kiasi kikubwa kushindwa kutoa maoni kuhusiana na hesabu hizo hivyo huleta mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa.

2.2 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

2.2.1 Idadi ya kaguzi zilizofanyika

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30 , 2018, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya kaguzi 255 za Serikali Kuu (Wizara na Taasisi, Hesabu Jumuifu za Taifa, Mamkala ya Mapato Tanzania , Sekretarieti za Mikoa, Wakala wa Serikali, Mifuko Maalum, Balozi, Bodi na Mamlaka za Maji, Taasisi zinginezo, Vyama vya Siasa); Mashirika ya Umma 122; Halmashauri 185 na Miradi ya Maendeleo 469.

2.2.2 Hati zilizotolewa

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa jumla ya Hati za Ukaguzi 1031. Kati ya hati hizo hati zinazoridhisha ni 989; hati zenye shaka 19; hati zisizoridhisha 17 na hati mbaya 6. Ufuatao ni mchanganuo wa idadi ya Hati zilizotolewa kwa mwaka husika,

Jedwali Na 3 : Muhtasari wa Hati zilizotolewa Mwaka 2017/18

Na.	Taasisi zilizokaguliwa	Idadi ya Taasisi zilizokaguliwa	Aina ya hati za ukaguzi			
			Hati zinazoridhisha	Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya
1.	Wizara, idara na Taasisi zake	255	237	11	2	5
2.	Halmashauri	185	176	7	1	1
3.	Mashirika ya Umma	122	121	1	0	0
4.	Miradi ya Maendeleo	469	455	0	14	0
Jumla		1031	989	19	17	6
Asilimia (%)			95.9%	1.8%	1.6%	0.6%

UNAAMBIWA KATIKA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA JUNI 30, 2018, OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ILIFANYA JUMLA YA KAGUZI 255!!!
MAPENDEKEZO YANAYOTOLEWA BAADA YA KAGUZI YANAFANYIWA KAZI?
MICHEZO
Man U' wins.

SURA YA TATU

3.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Sura hii inatoa tathimini ya utekelezaji wa mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa katika kaguzi za fedha zilizofanyika miaka iliyopita. Hii inajumuisha mapendekezo yaliyotolewa katika ukaguzi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Miradi ya Maendeleo.

3.1 Matokeo ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za fedha za miaka ya nyuma

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo imegawanyika katika makundi manne ikiwa ni mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu, ambayo utekelezaji umeanza, ambayo utekelezaji wake haujaanza kabisa na mapendekezo ambayo yamepitwa na wakati. Katika kupitia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi, tathimini inaonesha kuwa, mapendekezo 21,854 yaliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2016/17, katika mapendekezo hayo mapendekezo 7,971 sawa na asilimia 36.5 yametekelezwa kikamilifu, hii ni asilimia 28.3 ya mapendekezo yote. Mapendekezo 5,430 sawa na asilimia 24.8, utekelezaji wake unaendelea. Hata hivyo, mapendekezo 4,891 sawa na asilimia 22.4 utekelezaji wake haujaanza; na mapendekezo 3,186 sawa na asilimia 14.6 yamepitwa na wakati.

Pia imeonesha kuwa mapendekezo 376 sawa na asilimia 1.7 yamejirudia, hii imejitokeza upande wa Serikali za Mitaa. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika Jedwali Na. 3.1

Jedwali Na 3.1: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa miaka iliyopita

Aina ya Ripoti	Idadi ya Mapendekezo	Utekelezaji umekamilika	Utekelezaji unaendelea	Utekelezaji haujaanza	Yamepitwa na wakati	Yamejirudia
Mamlaka za Serikali za Mitaa	11,774	4,469	2,768	2,168	1,993	376
Mashirika ya Umma	112	52	36	18	6	0
Serikali Kuu	4,282	1,459	1,626	752	445	0
Miradi ya maendeleo	5,686	1,991	1,000	1,953	742	0
Jumla	**21,854**	**7,971**	**5,430**	**4,891**	**3,186**	**376**
Asilimia	***100***	***36.5***	***24.8***	***22.4***	***14.6***	***1.7***

Tathimini inaonesha kasi ya utekelezaji wa mapendekezo bado hairidhishi ingawa imeongezeka kwa asilimia 8.2 ikilinganishwa na ripoti ya mwaka ulioishia Juni 30, 2017. Tathimini inaonesha hali ya utekelezaji imeongezeka kwa kasi zaidi upande wa Serikali za Mitaa.


BILIONI 1.5 ZA MAKATO YA MISHAHARA HAJAZIFIKISHA TRA WALA HIFADHI YA JAMII
LABDA ALIIBIWA NJIANI JAMANI
HIC!
HAC!
HIC!
MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 41

SURA YA NNE

4.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2017/18

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha kwa taasisi 255 zilizokaguliwa zikiwemo Mafungu 65 ambayo hujumuisha Wizara na Taasisi; Sekretarieti za Mikoa 26; Wakala wa Serikali 33; Mifuko Maalum 16; Balozi za Tanzania 41; Bodi na Mamlaka za Maji 14; Taasisi nyinginezo 42; Mfuko jumuifu 2; Mamlaka ya Mapato Tanzania 2 na Vyama vya Siasa 14

4.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

4.1.1 Utekelezaji wa bajeti

Ukaguzi uliofanyika katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 ulibaini mapungufu katika ukusanyaji wa mapato ambapo Serikali haikufanikiwa kukusanya asilimia 12.66 ya makisio ya mapato.

Aidha, ukaguzi ulibaini asilimia 2.02 ya fedha za matumizi ya kawaida na asilimia 28.82 ya fedha za maendeleo hazikupokelewa.

Kutokana na mapungufu haya Serikali imeshindwa kutekeleza majukumu ya msingi ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Taarifa ya makusanyo imeoneshwa katika Jedwali Na. 4.

Jedwali Na. 4: Tofauti ya makisio na makusanyo halisi ya bajeti ya Serikali Kuu

Maelezo	Fedha za makusanyo ya mapato (Sh. Bilioni)	Fedha za matumizi ya Kawaida (Sh. Bilioni)	Fedha za matumizi ya Maendeleo (Sh. Bilioni)
Makisio ya fedha	31,711.99	20,278,99	11,432.99
Fedha zilizokusanywa/ pokelewa	27,695.96	15,408.03	7,219.26
Fedha zisizokusanywa/ pokelewa	4,016.03	317.13	2,923.00
Asilimia ya fedha zisizokusanywa/pokelewa	12.66	2.02	28.82

Chanzo: Muhtasari wa ripoti kuu 2018 (ukurasa wa xxvi - xxviii)

4.1.2 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu jumuifu (Hesabu za Taifa)

Ukaguzi ulibaini kasoro katika maeneo yafuatayo kwenye ukaguzi wa hesabu jumuifu za Taifa;

i) Kiasi cha shilingi bilioni 678 ambacho kilikusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa niaba ya Taasisi za Bodi za Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Bandari na Tozo ya Maendeleo ya Reli, Tozo za Korosho na Tozo za Ngozi zimeoneshwa kama sehemu ya mapato ya TRA kwenye hesabu jumuifu badala ya kuoneshwa kama mapato ya taasisi husika hivyo kusababisha mapato hayo kuripotiwa mara mbili kati ya TRA na taasisi hizo.

ii) Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 2.54 kilichokusanywa na Balozi 7 za Tanzania katika mwaka wa fedha 2017/18 hakikuwasilishwa

kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina kinyume na Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya Mwaka 2001. Badala yake, kiasi hicho cha fedha kilibakizwa katika akaunti za fedha za Balozi husika.

Mapendekezo: Serikali irejee hesabu jumuifu, kufanya marekebisho na ihakikishe kuwa tozo na mapato yaliyokusanywa na mamlaka kupitia akaunti maalumu za amana kwa niaba ya taasisi nyingine yanahamishwa kwa wakati kwenda kwenye taasisi husika ili kuziwezesha kutekeleza malengo na mipango iliyokusudiwa.

4.1.3 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania

i) Ilibainika kuwa, Mamlaka ya Mapato Tanzania ina mashauri ya kodi ya thamani ya shilingi trilioni 382.6. Kiasi cha shilingi trilioni 382 (asilimia 99.84) kimekwama katika Bodi ya Rufaa za kodi, shilingi bilioni 65.995 (asilimia 0.2) kimekwama katika Baraza la Rufaa za kodi, na kiasi cha shilingi bilioni 548. 31 (asilimia 0.14) kinasubiri maamuzi katika Mahakama ya Rufaa Tanzania. Pia mashauri manne(4) yenye thamani ya shilingi trilioni 374.7 yanayoihusu Kampuni ya Uchimbaji Madini ya ACACIA nayo yanasubiria maamuzi katika Mahakama ya Rufaa.

ii) Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishindwa kukusanya mapato zaidi ya shilingi bilioni 1.85 na dola za Marekani milioni 2.75 kutoka Mashirika ya Ndege 19, Mamlaka ya viwanja vya ndege Arusha na Kampuni ya Huduma za Meli kwa abiria wanaosafiri.

iii) Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishindwa kuthibitisha kulipwa kwa ongezeko la thamani ya kodi (VAT) ya shilingi bilioni 649.45 kwa bidhaa

zilizosafirishwa kutoka nchini kwenda nchi zingine zilizopaswa kutozwa kodi ya ongezeko la thamani. Bidhaa hizo ziliruhusiwa kwenda nje ya nchi bila kukamilisha taratibu za forodha kupitia mfumo wa TANCIS katika mipaka ya Mtambaswala, Hororo, Bandari za Mtwara na Tanga, kama taratibu za forodha zinavyotaka.

Mapendekezo: Serikali ifanye juhudi za makusudi kuziwezesha Mahakama za Rufaa za Kodi ili kuhakikisha mashauri ya kodi yanashughulikiwa kwa wakati ili kupunguza mrundikano wa mashauri. Serikali idhibiti mifumo ya ukusanyaji wa tozo za huduma za usafiri kwenye viwanja vya ndege na bandari.

Pia, Serikali iimarishe udhibiti wa mafuta na bidhaa zinazoingia nchini kwa matumizi ya ndani, na zinazopita kwenda nchi nyingine ili kuhakikisha kuwa zinalipiwa kodi stahiki.

4.1.4 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa deni la Taifa

Kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Deni la Taifa lilikuwa shilingi bilioni 50,926.51 ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 14,732.45 na deni la nje shilingi bilioni 36,194.06; kiasi hiki ni ongezeko la shilingi bilioni 4,845.08 sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 46,081.43 lililoripotiwa tarehe 30 Juni, 2017. Masuala yafuatayo yalibainika katika ukaguzi wa deni la taifa:

i) Usahihi wa taarifa unatia shaka kutokana na udhibiti wa ndani usiojitosheleza katika kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa za deni la Taifa.

ii) Serikali kuchelewa kulipa madeni ya Benki Kuu ya kiasi cha shilingi bilioni

212.7. Kati ya hizo, shilingi bilioni 199.79 zinatokana na riba ya nakisi ya Serikali, na shilingi bilioni 12.9 ni sehemu ya gharama za kudhibiti ukwasi kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18.

iii) Kutokuwapo kwa uwianishaji wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na Mfumo wa Utunzaji wa Taarifa za Deni la Taifa wa Jumuiya ya Madola (Common Wealth Secretariat-Debt Record Management System – (CS-DRMS)).

Mapendekezo: Serikali iimarishe udhibiti wa ndani katika kuhakiki mikopo iliyopokelewa na taasisi nufaika kabla ya kuingiza kumbukumbu za madeni kwenye mfumo ili kuondoa mapungufu katika usahihi wa taarifa.

4.1.5 Masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa awali wa malipo ya Pensheni yanayolipwa na Mfuko Mkuu wa Hazina

i) Kuchelewa kuandaliwa na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali majalada ya wastaafu 1,501 kati ya majalada 2,868 kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha chini ya mwaka mmoja hadi zaidi ya miaka minne (4).

ii) Majalada 69 yaliyorudishwa kwa waajiri kwa hoja yalikuwa hayajarudishwa kwa CAG kwa ajili ya kukaguliwa upya.

Ucheleweshaji wa kurudishwa majalada yaliyohojiwa, unasababisha kuchelewa kwa malipo ya hitimisho la kazi kwa wastaafu na wanufaikaji

iii) Kati ya majalada 2898, majalada 54 yalihohojiwa na kurudishwa kwa Maofisa Masuuli husika kwa ajili ya masahihisho. Majalada 295 yalibainika kukokotolewa kimakosa na kati ya hayo, 172 yalibainika kuwa na ziada ya malipo ya shilingi milioni 577.32 huku majalada 123 yakiwa na upungufu wa malipo ya shilingi milioni 294.35

Mapendekezo: Maafisa Masuuli waimarishe udhibiti na utaratibu wa kufanya mapitio ya uandaaji wa mafao ili kuhakikisha kuwa kanuni na vigezo vya ukokotoaji na sheria vinazingatiwa ili kuepuka ucheleweshaji wa mafao ya hitimisho la kazi na hasara kwa Serikali.

4.1.6 Mapungufu katika utendaji wa Wakala wa Serikali

i) Wakala za Serikali hazikupeleka kiasi cha shilingi bilioni 9.26 kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina kama inavyotakiwa na Kifungu cha 11 (3) cha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001.

ii) Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 57.09 ikiwa ni riba ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi wa ujenzi na washauri wa miradi.

iii) Kasi ndogo ya Wakala wa Majengo Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo yenye thamani ya shilingi bilioni 24.06.

iv) Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kuhamisha fedha zilizokuwa za tozo za wakandarasi na fedha za kodi ya zuio za kazi zenye jumla ya shilingi bilioni 6.65 kwenda Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Mapendekezo: Maafisa Masuuli wahakikishe wanaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, wanalipa wakandarasi wa ujenzi na washauri wa miradi kwa wakati na kuhamisha fedha kwenda Mfuko mkuu wa hazina. Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali zihamishe mali na madeni yote yanayohusiana na miradi ya barabara kwenda Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini.

4.1.7 Mapungufu katika utengenezaji wa vitambulisho vya Taifa kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Kati ya watu 19,662,105 ni watu 4,511,809 ambao vitambulisho vyao vilitengenezwa ikiwa ni sawa na asilimia 23 chini ya Kampuni ya IRIS Corporation Berhard ya Malaysia ambayo kwa sasa imesimamisha shughuli zake zote za utengenezaji vitambulisho kuanzia tarehe 14 Machi 2018 kwa sababu za kutokulipwa Dola za Kimarekani milioni 30.18 sawa na shilingi bilioni 69.98.

Mapendekezo: Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iharakishe zoezi la usajili na utengenezaji wa vitambulisho vya Taifa. Pia, itathmini utendaji kazi wa mkandarasi ili kuweza kuamua iwapo imuongezee muda wa mkataba au iingie makubaliano na mkandarasi mwingine.

4.1.8 Mapungufu katika usimamizi wa manunuzi na mikataba

i) Kiasi cha shilingi bilioni 4.61 kilitumika kununua bidhaa, huduma na kazi za ujenzi ndani bila kutumia taratibu za kushindanisha wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni za 163 na 164 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

ii) Taasisi saba (7) zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 5.37 bila kupata vibali vya Bodi za Zabuni kinyume na Kifungu cha 35 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, na Kanuni 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

iii) Taasisi tano (5) zilifanya manunuzi ya bidhaa, huduma, na kazi za kiasi cha shilingi bilioni 1.17 bila kuwapo kwa makubaliano ya kimkataba na Wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni Namba 10 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

Mapendekezo: Maafisa Masuhuli wahakikishe sheria na kanuni za manunuzi zinafuatwa.

4.1.9 Mapungufu katika usimamizi wa Matumizi

i) Matumizi ya shilingi bilioni 4.66 yalifanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kampuni binafsi za huduma za kisheria bila kufuata makubaliano ya mikataba.

ii) Taasisi 20 za Serikali Kuu ziliwalipa watoa huduma mbalimbali kiasi cha shilingi bilioni 1.43 pasipo kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD).

iii) Malipo yalifanyika kimakosa katika vifungu visivyostahili ya kiasi cha shilingi bilioni 885.99 kinyume na Kanuni ya 42(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001.

Mapendekezo: Maafisa Masuhuli wahakikishe sheria na kanuni za usimamizi wa matumizi ya fedha zinafuatwa.

HIZI NI GARI ZA HALMASHAURI NA ZOTE ZILINUNULIWA MPYA!
Pesa ZA WALIPA KODI ZINAOZEA HAPA!

SURA YA TANO

5.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Sura hii inatoa muhtasari na majumuisho kuhusu ukaguzi wa taarifa za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) 185 zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2017/18.

5.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA

Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2018 ulibaini mapungufu katika maeneo yafuatayo:

Utekelezaji wa bajeti

i. Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 hazikukusanya kiasi cha shilingi bilioni 111.24 sawa na asilimia 16 ya bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi bilioni 677.97. Hii inaonesha kwamba bajeti ya mapato ya ndani inaandaliwa bila kufanya upembuzi yakinifu.

ii. Kutolewa zaidi kwa ruzuku ya miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 yenye jumla ya shilingi bilioni 22.06 sawa na asilimia 26 ya bajeti iliyoidhinishwa. Halmashauri zilizoongoza kwa kupata asilimia kubwa zaidi ni Halmashauri ya Mji wa Newala ilipata asilimia 3,202, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba ilipata asilimia 129 na Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ilipata asilimia 124.

iii. Mamlaka za Serikali za mitaa 20 zilipokea ruzuku ya matumizi ya kawaida zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 42.64 sawa na asilimia 9. Halmashauri zilizoongoza kwa kupata asilimia kubwa zaidi ni Halmashauri ya wilaya ya Mpimbwe asilimia 37, Halmashauri ya Mji wa Mbinga asilimia 29

na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero asilimia 25. Hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha zilizotolewa zaidi.

iv. Kutolewa kiasi pungufu cha ruzuku ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 156, jumla ya shilingi bilioni 480.01 sawa na asilimia 49 ya jumla ya bajeti iliyoidhinishwa. Hii inamaanisha shughuli za miradi ya maendeleo zilizokuwa kwenye mpango hazikutekelezwa.

v. Kutolewa kiasi pungufu cha ruzuku ya matumizi ya kawaida katika Mamlaka za Serikali za 165, jumla shilingi bilioni 987.89 sawa na asilimia 20 ya bajeti iliyoidhinishwa.

vi. Ruzuku ya matumizi ya kawaida jumla ya shilingi bilioni 139.56 sawa na asilimia 3 ya fedha zilizopokelewa hazikuweza kutumika hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 174.

vii. Ruzuku ya maendeleo jumla ya shilingi bilioni 261.45 sawa na asilimia 33 ya fedha zilizopokelewa haikuweza kutumika hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 176.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha upatikanaji wa fedha kutoka kwenye vyanzo vya ndani ikiwa ni pamoja na kukuza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa fedha. Vilevile Serikali inashauriwa kupeleka fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Mapungufu katika Usimamizi wa Rasilimali watu na mishahara

i. Kuwepo kwa madai mbalimbali ya watumishi na malimbikizo ya mishahara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 22 ambayo hayajalipwa yenye jumla ya Shilingi bilioni 11.14

ii. Malipo ya mishahara na makato ya kisheria kwa taasisi mbalimbali yanayohusisha watumishi ambao hawako kwenye utumishi wa Umma shilingi milioni 207.38 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17.

iii. Kuchelewa kuidhinisha upandishwaji vyeo na ongezeko la mishahara kwa watumishi 10,899 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17.

iv. Makato ya mishahara kiasi cha shilingi bilioni 1.05 hayakuwasilishwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na taasisi nyingine katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 41.

v. Malipo kwa watumishi wa muda mfupi kiasi cha shilingi milion 210.10 yalifanyika bila kuwepo kwa mikataba halisi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa tano (5).

Mapendekezo: OR-TAMISEMI, OR-Menejimenti Utumishi wa Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili kutatua masuala mbalimbali yaliyojitokeza ili kufikia ufanisi katika usimamizi wa rasilimali watu. Pia Serikali isimamie utekelezaji wa maslahi ya watumishi, ajira, mafunzo, tathmini ya utendaji na upandishaji vyeo ili kufikia mafanikio yaliyotarajiwa.

5.2 Mapungufu katika usimamizi wa mikataba na manunuzi

i. Manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.94 yalifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 48 bila kushindanisha wazabuni. Hali hiyo inatia shaka kama thamani ya fedha ilipatikana katika Halmashauri zilizofanya manunuzi hayo.

ii. Manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 9.05 yalifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 32 bila kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Halmashauri ya wilaya ya Newala iliongoza kwa kuwa na kiasi kikubwa cha shilingi bilioni 5.65 sawa na asilimia 62, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chemba yenye kiasi cha shilingi bilioni 1.25 sawa na asilimia 14.

iii. Bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi milioni 923.84 zilinunuliwa kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18.

iv. Ununuzi wa bidhaa mbalimbali na huduma zenye thamani ya shilingi milioni 471.41 kwa kutumia masurufu ulifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18.

v. Bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 1.41 zilipokelewa bila kukaguliwa na kamati za ukaguzi na mapokezi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 31. Kupokea bidhaa zilizonunuliwa bila kufanyiwa ukaguzi thabiti kunaweza kusababisha mapokezi ya bidhaa pungufu, zisizoendana na viwango tarajiwa na za bei ya juu kinyume na mkataba wa mauziano.

vi. Manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 28.54 yalifanyika nje ya mpango wa manunuzi wa mwaka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 14.

Hali hii inapelekea kutokufanyika kwa manunuzi yaliyopangwa na thamani ya fedha katika manunuzi ya namna hii haiwezi kupatikana.

vii. Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 zilinunua bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 1.57 ambazo hazikuingizwa kwenye leja ya vifaa. Hali hii inazuia mawanda ya ukaguzi katika kujiridhisha iwapo vifaa vilivyonunuliwa vilipokelewa na kutumika kama inavyostahili.

viii. Kuondolewa kwa wazabuni kumi na tatu (13) wenye bei ya chini bila sababu za msingi na kusababisha hasara ya shilingi bilioni 2.37 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 4. Halmashauri ya Manispaa ya Songea iliongoza kwa kuwa na kiasi cha shilingi bilioni 1.93 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo yenye kiasi cha shilingi milioni 222.72

ix. Mikataba 20 yenye thamani ya shilingi bilioni 24.85 ilitekelezwa bila kuwepo na dhamana ya utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi 10. Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto iliongoza kwa kuwa na kiasi cha shilingi bilioni 6.80 ikifuatiwa na Halmashauri ya Mji wa Nzega yenye kiasi cha shilingi bilioni 5.79, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala yenye kiasi cha shilingi bilioni 4.31 na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke yenye shilingi bilioni 3.79.

x. Bidhaa na huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 15 zenye thamani ya shilingi milioni 573.04 zililipiwa lakini hazikupokelewa.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuhakikisha kuwa Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na Kanuni zake zinazingatiwa.

Pia kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika utaratibu mzima wa manunuzi, na hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya watumishi wote waliovunja sheria za manunuzi na kusababisha hasara.

5.3 Tathmini ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma

i. Malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 6.72 yalifanyika yakiwa na nyaraka pungufu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 106. Hii imepelekea kushindwa kuthibitisha uhalali na ukamilifu wa malipo hayo.

ii. Hati za malipo zenye jumla ya shilingi bilioni 1.64 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 hazikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi. Halmashauri za wilaya ya Nyang'hwale ilifanya malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 1.05 sawa na asilimia 64 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe yenye kiasi cha shilingi milioni 277.43 sawa na asilimia 17.

iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa 20 zilifanya matumizi ya shilingi milioni 720.41 pasipo Serikali kupata huduma wala manufaa yoyote. Matumizi hayo yanajumuisha gharama za tozo, adhabu au riba kwa kushindwa kuzingatia vipengele vya mikataba kwa Wakandarasi na posho kwa watumishi kwa kazi ambazo hazikufanyika.

iv. Mamlaka za Serikali za Mitaa 48 zilifanya malipo kiasi cha shilingi bilioni 1.998 katika vifungu visivyo sahihi. Hii inaweza kusababisha kuongezeka au kupungua kwa matumizi katika vifungu husika.

v. Malipo ya shilingi bilioni 3.94 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 41 yamefanyika bila kufanyiwa ukaguzi wa awali. Kuna uwezekano mkubwa wa kukosa viambatanisho vya kutosha, kutoidhinishwa na kuweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Umma.

vi. Malipo ya takribani shilingi bilioni 5.01 yalifanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 46 nje ya bajeti. Hii inatokana na kuandaa bajeti isiyo sahihi na udhibiti duni wa vifungu vya bajeti.

vii. Kutorejeshwa kwa madeni ya ndani kati ya akaunti moja kwenda akaunti nyingine (vifungu na vifungu) yenye thamani ya shilingi bilioni 2.61 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 13.

viii. Malipo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.03 yalifanyika bila kuidhinishwa na Wakuu wa Idara na Maafisa Masuuli katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17.

ix. Madeni kiasi cha shilingi bilioni 4.698 kutoka Akaunti ya Amana hayakurejeshwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 73. Halmashauri ya Wilaya ya Ngara inaongoza kwa kuwa na jumla ya shilingi milioni 392.65 ikifuatiwa na Halmashauri ya wilaya ya Bumbuli yenye jumla ya shilingi milioni 281.08.

x. Malipo kiasi cha shilingi bilioni 6.96 yalikosa uthibitisho wa fedha zake kuwapo katika akaunti ya amana katika Serikali za Mitaa 45. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe inaongoza kwa kuwa na jumla ya shilingi bilioni 1.64 ikifuatiwa na Halmashauri ya wilaya ya Kilombero yenye jumla ya shilingi milioni 434.26.

xi. Mamlaka za Serikali za Mitaa 74 zilifanya malipo ya jumla ya shilingi bilioni 8.51 kwa wakandarasi na watoa huduma mbalimbali bila kudai stakabadhi za kielektroniki (EFD) ambapo Halmashauri ya Mji wa Bariadi ilibainika kulipa kiasi cha shilingi bilioni 2.24, ikifuatiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Mji wa Korogwe ambazo zilishindwa kudai stakabadhi zenye thamani ya shilingi milioni 963.56 na 827.05 mtawalia.

xii. Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 zilifanya malipo ya shilingi bilioni 1.21 kwa wadai ambao hawakuoneshwa kwenye taarifa za fedha za mwaka uliopita.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zinanashauriwa kuimarisha udhibiti wa matumizi ili kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumiwa kama zilivyokusudiwa kwa kuzingatia kiasi kilichoidhinishwa, na kufuata kanuni za usimamizi wa fedha za umma.

5.4 Utekelezaji wa elimu bila malipo

Katika kutekeleza mwongozo wa elimu bila malipo, serikali haikuweza kupeleka kiasi cha shilingi bilioni 2.44 mashuleni kwa ajili ya ruzuku ya matumizi kwa shule za Msingi na hii ni asilimia 20 ya kiasi kilichokadiriwa cha shilingi bilioni 12.33 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18. Jambo hili ni kinyume na mwongozo wa utekelezaji wa elimu bila malipo.

Mapendekezo: Serikali inashauriwa kutoa fedha kulingana na bajeti iliyopitishwa ili kutengeneza mazingira mazuri ya elimu kwa walimu na wanafunzi na hivyo kuongeza ufanisi katika elimu na hatimaye kufanikisha malengo yaliyowekwa.

5.5 Mapungufu katika usimamizi na udhibiti wa mapato ya ndani

i. Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 hazikukusanya ushuru wa huduma wa asilimia 0.3 ya mauzo ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani kutoka katika makampuni 8,613 yanayoendesha shughuli zake katika maeneo husika.

ii. Mashine 56 za kielektroniki za kukusanyia mapato (PoS Machine) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 7 hazikusajiliwa wala kuonekana katika Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS).

iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa 8 zilikuwa na mawakala 195 wa kukusanya mapato kutoka vyanzo vya ndani bila kuwa na mikataba ya makubaliano ya kisheria.

iv. Mamlaka ya Serikali za Mitaa 7 zimefanya marekebisho kwenye mfumo wa mapato ya jumla ya shilingi bilioni 35.83 bila uwapo wa nyaraka za kuthibitisha marekebisho hayo.

v. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 78 kulikuwa na makusanyo ya mapato ya shilingi bilioni 5.27 kutoka vyanzo mbalimbali ambayo hayakuthibitishwa kupelekwa benki.

vi. Marekebisho ya ankara yenye thamani ya shilingi bilioni 9.43 katika Halmashauri 50 yaliombwa na kuidhinishwa na mtu mmoja katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato (LGRCIS). Hii ni kinyume na utaratibu wa udhibiti wa ndani katika ugawaji wa majukumu.

Mapendekezo: Serikali inashauriwa ifanye jitihada za kuboresha mfumo wa taarifa wa ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa (LGRCIS) kwa kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoukabili mfumo huo ili kuweza kuboresha ukusanyaji wa mapato. Pia Halmashauri zihakikishe makusanyo ambayo hayakupelekwa benki yanapelekwa mara moja.

5.6 Mapungufu katika usimamizi wa mali

i. Magari, mitambo na pikipiki 504 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 97 yamekaa muda mrefu bila kutumika na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. Hii huongeza gharama za matengenezo ambayo husababishwa na mali hizo kuharibika zaidi na pia kupunguza thamani ya soko ambayo ingepatikana endapo mali hizo zingeondolewa na kuuzwa mapema.

ii. Madawa yenye thamani ya shilingi milioni 276.89 yako katika stoo za Halmashauri 6 kwa vipindi mbalimbali kuanzia mwaka 1990 hadi 2018 bila kuteketezwa.

iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa 9 zimethaminisha ardhi yenye thamani ya shilingi bilioni 25.71 na kuzijumuisha katika taarifa zao za fedha bila kufanya jitihada za kupata hatimiliki.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kufanya tathmini ya mali zote ambazo zimekaa muda mrefu bila kutumika/zilizotelekezwa ili kufanya uamuzi wa kuziondoa au kuzifanyia matengenezo. Vilevile Mamlaka za Serikali za Mitaa 9 zilizothaminisha ardhi yenye thamani ya shilingi bilioni 25.71 na kuzijumuisha katika taarifa zao za fedha zihakikishe zinapata hati miliki za ardhi kutoka kwa Mamlaka husika.

5.7 Mapungufu katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

i. Miradi 27 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.24 ilikamilika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 16, lakini haitumiki. Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara iliongoza kwa kuwa na miradi ya shilingi bilioni 1.96.

ii. Kiasi cha shilingi bilioni 5.02 zilitumika kwenye shughuli zisizokusudiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 40.

iii. Miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 41.495 haikutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 30 kama ilivyokuwa imepangwa kutokana na kutopokea fedha kutoka Serikali Kuu au makusanyo hafifu ya mapato ya ndani. Pia kazi za miradi ya maendeleo zenye thamani ya shilingi bilioni 8.27 hazikutekelezwa licha ya kuwepo na fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 18.

iv. Usimamizi hafifu wa miradi, umesababisha kutokamilika kwa miradi ya maendeleo na kutelekeza miradi kwa muda mrefu, miradi hiyo yenye thamani ya shilingi bilioni 52.43 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 47.

v. Mamlaka za Serikali za Mitaa 62 hazikupeleka asilimia 20 ya ruzuku iliyopokelewa kutoka Serikali Kuu yenye jumla ya shilingi bilioni 3.32 kwenye ngazi za chini (vijiji, mitaa, kata) ikiwa ni fidia ya vyanzo vya ndani vya mapato vilivyofutwa,

Mapendekezo: Serikali ifikirie kuweka utaratibu ambao utahakikisha kuwa miradi ya maendeleo inatengewa rasilimali fedha za kutosha na fedha zinatumika kwa wakati kutekeleza miradi ya maendeleo. Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe miradi

ambayo haijakamilika na iliyotelekezwa inakamilishwa, miradi yote iliyokamilika inatumika na asilimia 20 ya ruzuku ya serikali kuu kwenda ngazi za chini (vijiji, Mitaa na kata) inapelekwa kwa wakati.

5.8 Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana

i. Mamlaka za Serikali za Mitaa 143 hazikuchangia asilimia 10 ya mapato yao ya ndani sawa na shilingi bilioni 40.38 katika Mfuko wa Wanawake na Vijana.

ii. Mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.04 iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake na vijana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 90 haikurejeshwa.

Mapendekezo: Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuchangia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana, kuongeza juhudi katika urejeshaji wa mikopo ili kufanikisha malengo. Pia zinashauriwa kuazisha mikakati ya uhakika itakayochochea wakopaji kurejesha mikopo kwa hiari ili kusaidia ukuaji endelevu wa mfuko huu.


DART
UNAONA UNACHOPASWA KUONA AU ANACHOTAKA UONE?
UDART

SURA YA SITA

6.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA

Sura hii inahusu muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Ripoti hii imeainisha masuala mbalimbali yanayoathiri utendaji wa Mashirika ya Umma na mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha utendaji na kufanikisha malengo waliyojiwekea.

6.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma

Katika ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma, mapungufu mbalimbali yalibainika kama ifuatavyo:

6.2 Mashirika Yasiyo na Uhakika Katika Utoaji Huduma kwa Siku za Usoni

Mashirika 14 ya Umma yana changamoto za kifedha pamoja na kupata hasara ambayo imesababisha madeni kuwa zaidi ya mitaji yao. Kati ya Mashirika hayo, Mashirika 11 yamekuwa yanajiendesha kwa hasara kwa zaidi ya miaka 2. Kwa hali hii, Mashirika haya yanakuwa tegemezi kwa msaada kutoka Serikali Kuu ili kujiendesha.

Mapendekezo: Serikali ifanye mapitio ya namna ya uendeshaji wa Mashirika haya na kuongeza mitaji ili yaweze kumudu gharama za uendeshaji.

6.3 Kuwepo kwa Wadaiwa Sugu wa Pango

i. Wapangaji 623 wameendelea kupokea huduma ya upangaji katika Kituo cha Mikutano cha Arusha (AICC) licha ya kuwa na madeni sugu yanayofikia Shilingi bilioni 3.80.

ii. Shirika la Bima la Taifa (NIC) limeripoti madai kiasi cha Shilingi bilioni 53, deni halisi ni shilingi bilioni 63 Madeni hayo yana upungufu wa thamani halisi kwa kiasi cha Shilingi bilioni 10. Kuna uwezekano kuwa mapato yaliyorekodiwa hayakuwa halisi. Hii ni kwa kuwa ukusanyaji wa madai hayo umekuwa mgumu, hivyo unaweza kusababisha hasara kutokana na mrundikano wa madai hayo.

Mapendekezo: Mashirika husika yanatakiwa kutekeleza sera zao za upangaji na usimamizi wa madeni ili kuwa na usimamizi imara wa mapato.

6.4 Madai Makubwa Kutoka kwa Watoto Tegemezi Wasiostahili

Malipo ya Shilingi bilioni 13.99 yamefanyika kwa vituo vya tiba kwa ajili ya watoto tegemezi ambao wamefikia umri wa miaka 18. Hii ni kinyume na Sheria ya NHIF.
Malipo hayo yamesababisha upotevu wa fedha za NHIF ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo.

Mapendekezo: NHIF ihuishe kanzi data yake ili kuwatambua watoto tegemezi waliozidi umri na kuweka udhibiti ambao utahakikisha hawahudumiwi tena na bima.

6.5 Kutopatikana kwa Wanufaika wa Mikopo

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeshindwa kuwapata wanufaika wa mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.46. Kutopatikana kwa wanufaika wa mikopo hii kunapunguza uwezo wa Bodi kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea.

Mapendekezo: HESLB ishirikiane na taasisi nyingine na vyanzo vingine vya taarifa kuboresha kanzi data yake ili kuwatambua wanufaika wa mikopo ambao bado hawajatambulika.

6.6 Kutegemea zaidi Wahisani wa Maendeleo katika Kufanikisha Shughuli za Msingi za Taasisi

Katika mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30 2018, bajeti ya NBS iliwezeshwa na Serikali kwa Shilingi bilioni 1.64 bila kuhusisha mishahara wakati Shilingi bilioni 13.84 iliwezeshwa na wahisani kupitia Mradi wa Mpango wa Kitakwimu Tanzania (TSMP). Hivyo kiwango kikubwa cha shughuli kuu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinafadhiliwa na wahisani. Mradi wa TSMP ulikuwa wa miaka 7 iliyoishia tarehe 30 Juni 2018.

Mapendekezo: Serikali iongeze uwezeshaji wa bajeti ya NBS ili iweze kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

6.7 Kutofautiana kwa Taarifa za Tozo kwa ajili ya Maegesho ya meli kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mamlaka ya Bandari Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania inakusanya tozo za maegesho ya meli kwa niaba ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na kila mwisho wa mwezi Mamlaka ya Bandari Tanzania inafanya uwianishaji wa kibenki. Hata hivyo, imegundulika kuna tofauti ya Shilingi bilioni 42.5 kati ya kumbukumbu za Mamlaka ya Bandari na zile za Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hii inatokana na ukosefu wa ushirikiano wa kutosha kati ya Mamlaka hizi mbili katika uwianishaji wa taarifa pindi inapotokea tofauti.

Mapendekezo: Mamlaka ya Bandari iboreshe usuluhishi wa kibenki kwenye tozo za maegesho ya meli ili kuhakikisha ufanisi na usahihi. Pia Mamlaka ya Bandari ihakikishe kuwa tofauti za kimahesabu zinafanyiwa marekebisho kwa wakati.

6.8 Mashirika ya Umma Kutokuwa na Bodi za Wakurugenzi

Katika ukaguzi wa mwaka 2017/18, Mashirika ya Umma 24 hayakuwa na Bodi za

Wakurugenzi. Kati ya Mashirika haya; saba (7) yanafanya kazi bila ya kuwa na bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja, huku Mashirika manne (4) yakiwa na zaidi ya miaka miwili. Kukosekana kwa Bodi za Wakurugenzi kunazorotesha udhibiti wa ndani na kuchelewesha utekelezaji wa baadhi ya shughuli za kiutendaji zinazohitaji idhini ya bodi katika Mashirika hayo.

Mapendekezo: Mamlaka ya uteuzi ichukue hatua stahiki, ikiwamo kuanza mapema mchakato wa kuteua kabla ya kuisha muda wa Bodi zilizopo.

6.9 Kuruhusu Bidhaa za Chakula Zilizomalizika Muda wake wa Matumizi na Zilizobakiza Muda Mfupi wa Matumizi

Uchunguzi wa sampuli za bidhaa za chakula uliofanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ulionesha kuwa kuna bidhaa zilizoisha muda wa matumizi ambazo zilisambazwa sokoni na kutumika. Hali hii inawaeza kuathiri afya za walaji.

Mapendekezo:TBS ihakikishe bidhaa zilizoisha muda haziruhusiwi kwa matumizi ya binadamu na ichunguzwe namna ambavyo bidhaa zilizoisha muda wake zilifaulu ukaguzi na kuruhusiwa kwenda kwenye matumizi na hatua stahiki zichukuliwe.

6.10 Kuchelewa kuendeleza Kanda Maalum za Uwekezaji kwa sababu ya Kutokamilisha Fidia ya Maeneo

Mamlaka ya Ukanda wa Kutengeneza Bidhaa za Kuuza Nje ya Nchi (EPZA) ilichelewa kulipa fidia ya maeneo yaliyopangwa kuendeleza Ukanda Maalum wa Uchumi (SEZ) ya Kituo cha Biashara na Usafirishaji cha Kurasini, Bagamoyo, Tanga, Ruvuma na Manyoni, wakati uhakiki na uthaminishaji wa maeneo ulishafanywa na Mthamini Mkuu wa Mali za Serikali. Katika kipindi cha miaka nane, ni kiasi cha Shilingi bilioni 34.2 tu zilizolipwa kutoka kiasi cha Shilingi bilioni 67.2 kilichopaswa kulipwa.

Mapendekezo: EPZA ilipe kiasi cha fedha kilichobaki ili iweze kuendeleza Maeneo Maalum ya Uwekezaji ya Kanda.

6.11 Ongezeko la Madeni ya Wafanyakazi katika Taasisi za Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu

Madeni yanayohusu malipo ya posho ya kujikimu kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Ardhi yameongezeka kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2017/18. Katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, madeni yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1.49 hadi shilingi bilioni 3.41, na kwa Chuo Kikuu cha Ardhi, madeni yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1.48 hadi bilioni 2.26. Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Mzumbe vilikuwa na madeni ya kiinua mgongo ya shilingi bilioni 5.59 na shilingi milioni 525, mtawalia kwa wafanyakazi ambao wamemaliza mikataba yao.

Vilevile, kumekuwa na madeni ya Shilingi bilioni 6.78 katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine ikiwa ni posho za nyumba na madeni mengineyo ya wafanyakazi tangu Juni 2017. Hali hii inaweza kusababisha kushuka kwa kiwango cha elimu ya juu kutokana na wahadhiri kukosa morali ya kazi.

Mapendekezo: Serikali ikamilishe mchakato wa uhakiki wa madeni hayo na kuweza kuyalipa madeni husika kwa wakati.

6.12 Ucheleweshaji wa Ukamilishaji wa Miradi ya Nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lilianzisha Mradi wa Nyumba wa Golden Premier Residence, Kitalu Na. 711/2 mnamo tarehe 16 Oktoba 2013. Mradi huo ulisimama tangu mwanzo mwa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Hadi mradi

unasimama ulikuwa umekamilika kwa asilimia 30 na umetumia Shilingi bilioni 34.87 kutoka vyanzo vya ndani na mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB). Shirika la Nyumba lilitakiwa kuanza kulipa marejesho ya mkopo huo kuanzia Julai 2018. Shirika linatumia vyanzo vingine vya fedha kulipa mkopo huo huku mradi ukiwa haujakamilika. Shirika limefikia ukomo wake wa kukopa na kama halitapata kibali cha kukopa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango litapaswa kuwalipa wakandarasi jumla ya Shilingi bilioni 99.99 kwa kuvunja mkataba. Pia, litatakiwa kuwarejeshea wateja waliokwishaanza kulipia malipo ya awali ya ununuzi wa nyumba hizo jumla ya Shilingi bilioni 2.6.

Mapendekezo: Wizara ya Fedha na Mipango iangalie namna bora ya kuepusha hasara inayoweza kupatikana kutokana na kutokukamilika kwa mradi wa Nyumba wa Golden Premier Residence.

6.13 Kupungua kwa Akiba ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), mwaka hadi mwaka, malipo ya huduma za afya yanakua kwa kasi kubwa zaidi ya kukua kwa mapato ya mwaka hadi mwaka ya mfuko. Kutokana na hali hii, mwelekeo unaonesha kuwa ifikapo mwaka wa fedha utakaoishia Juni 2024, malipo ya huduma za bima ya afya yanakisiwa kufikia asilimia 99.2 ya makusanyo yote. Uwiano huu unakisiwa kuongezeka kufikia asilimia 104.8 katika mwaka utakaofuata wa fedha. Hali hii inamaanisha kuwa kipindi ambapo makusanyo na mapato kutoka katika uwekezaji hayataweza kukidhi madai ya huduma za bima ya afya na hivyo itaulazimu mfuko kuchukua hatua za dharura kama kuuza mali zake.

Mapendekezo: NHIF inashauriwa iwe na udhibiti na ufuatiliaji kuhusu kukuwa kwa kiwango cha madai ya huduma za bima ya afya.

6.14 Ucheleweshaji wa Makusanyo ya Madeni Katika Mamlaka za Maji Shilingi bilioni 97.58

Kumekuwepo na kiwango kidogo cha kukusanya marejesho ya madeni ndani ya Mamlaka za Maji. Mapato mengi hayajakusanywa na yamezidi muda uliowekwa kwenye Sera za Mikopo za Mamlaka husika. Katika jumla ya deni la Shilingi bilioni 97.58 lililobainika, Shilingi bilioni 39.59 (sawa na asilimia 41) ni Madeni ya Serikali na Shilingi bilioni 57.99 (sawa na asilimia 59) ni madeni ya wateja wengine. Ongezeko hili limesababishwa na ufuatiliaji hafifu wa wadeni na kutokufuata Sera ya Mamlaka za Maji ya kukata huduma za maji kwa wateja wanaokiuka taratibu. Jambo hili hupunguza uwezo wa kifedha wa Mamlaka hizo za Maji na kuathiri shughuli.

Mapendekezo: Mamlaka za Maji zinahitaji kuainisha mipango ya ukusanyaji wa madeni na kuisimamia mipango hiyo kwa ukaribu.

6.15 Udhaifu katika Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi katika Mashirika ya Umma

i. Mnamo mwaka 2015, Kampuni Hodhi ya Kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli (RAHCO) ilifanya malipo ya awali kiasi cha Dola za Marekani 500,000 (sawa na Shilingi bilioni 1.07) kwa mhandisi mshauri kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge). Hadi kufikia Februari 2019, huduma hiyo haikutolewa, ikiwa ni miaka mitatu tangu malipo yalipofanyika. Mkataba ulisainiwa tarehe 20 Mei, 2015 na ulikuwa wa miezi kumi na mbili. Kwa mujibu wa menejimenti ya RAHCO, suala hili lipo mahakamani kwa ajili ya hatua za kisheria.

ii. DAWASA iliingia mkataba na kampuni ya Serengeti ili kuchimba visima ishirini (20) vyenye thamani ya Shilingi bilioni 19.82 katika eneo la Kimbiji na Mpera.

Kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi alitakiwa kulipa fidia ya Shilingi bilioni 1.98 ambayo ni asilimia 10 ya thamani ya mkataba kwa kuchelewesha kazi kwa muda wa siku 200.Udhaifu uliobainika unaweza kusababisha upotevu wa fedha ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyingine za maendeleo.

Mapendekezo: Mashirika husika yanashauriwa kufanya jitihada ili fedha husika zirejeshwe na zitumike katika shughuli nyingine za maendeleo.

6.16 Malipo Hewa kwa Mzabuni yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Uchunguzi ulibaini malipo hewa ya Shilingi bilioni 3 yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Malipo haya yalitakiwa kufanyika kwa watoa huduma kwa kutumia hundi zilizofungwa lakini yalifanyika kwa fedha taslimu kinyume na Kanuni za Fedha za NHIF. Uchunguzi umebaini pia kuwa wafanyakazi wanne wa NHIF walihusika na kupokea malipo hayo kutoka benki. Suala hili limesababisha ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma.

Mapendekezo: Mamlaka husika ichukue hatua zinazofaa dhidi ya wafanyakazi wanaohusika katika ubadhirifu uliobainishwa.

6.17 Mapungufu katika Uendeshaji wa Mradi wa Mwendokasi

Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa mwendokasi, kampuni ya UDART ilinunua mabasi 140 badala ya 305 yaliyotakiwa. Mabasi yaliyonunuliwa ni sawa na asilimia 45.9 ikiwa ni pungufu kwa mabasi 165, sawa na asilimia 54.1. Hii inaleta changamoto ya mrundikano wa abiria hivyo mabasi yanajaa sana na hivyo kuongeza kasi ya uchakavu. Pia, kadi za malipo za UDART zimesitishwa kwasababu gharama za uzalishaji ni kubwa kuliko mauzo yake kwa abiria wa mwendokasi.

Imebainika kuwa gharama za kuzalisha kadi moja ni Shilingi 4,500 wakati Serikali ilitangaza kadi moja kuuzwa Shilingi 500. Hii imesababisha kuendelea kutumia tiketi za kawaida ambapo inaweza kuleta upotevu wa mapato.

Mapendekezo: Inapendekezwa kampuni ya UDART iongeze idadi ya mabasi ili kukidhi mahitaji ya sasa na pia Serikali itafute ufumbuzi juu ya suala la kadi ili kuzuia upotevu wa mapato unaoweza kutokea.

6.18 Msukumo Mdogo katika Kutekeleza Maelekezo ya Iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini

Kampuni ya Mafuta ya Taifa TPDC, iliomba leseni ya utafiti wa mafuta na gesi katika vitalu Na. 4/1B na 4/1C kutoka kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini. Mnamo mwaka 2015, Wizara iliielekeza TPDC kuongeza thamani ya vitalu husika, kufanya tathmini ya kitakwimu na kiuchumi na kuishauri Wizara. Mpaka kufikia mwaka 2017, pamoja na thamani kuongezwa na tathmini kufanyika, Wizara haikuwa imepokea ripoti ya vitalu husika kutoka TPDC huku TPDC ikiendelea kuomba leseni ya uchunguzi wa mafuta na gesi. Kwa TPDC kushindwa kutekeleza maelekezo ya Wizara kunamfanya Waziri aendelee kuchelewa kutoa idhini na utaratibu wa kuipa TPDC vitalu husika.

Mapendekezo: TPDC iwasilishe Wizara ya Nishati ripoti inayohusiana na kuongeza thamani na tathmini ya vitalu 4/1B na 4/1C ili Wizara ili Wizara iweze kutoa maamuzi.

SERI
KALI
MIRADI YA
MAENDELEO

SURA YA SABA

7.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO

Sura hii inahusu muhtasari wa majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Miradi ya maendeleo inajumuisha miradi mikubwa minne inayofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wahisani kupitia mfuko wa pamoja. Miradi minne ya maendeleo ambayo huchangiwa kwa pamoja ni Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP), Mfuko wa Afya (HBF), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Programu ya Maendeleo Sekta ya Maji (WSDP). Aidha, ukaguzi umefanyika katika miradi mingine inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa (UN) na wadau wengine wa maendeleo.

7.1 MATOKEO YA UKAGUZI

7.2 Uchangiaji usioridhisha wa Serikali katika Miradi ya Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ilitakiwa kuchangia shilingi bilioni 118.44 katika miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018 Serikali ilichangia shilingi bilioni 7.43 sawa na asilimia 6 na hivyo kushindwa kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 111.01 kinyume na makubaliano na wadau wa maendeleo.

Mapendekezo: Serikali itafute sababu zinazopelekea Serikali kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kuchangia miradi husika kutokana na makubaliano na pia kutafuta njia ya kutatua changamoto hii.

7.3 Utekelezaji wa Miradi ya Umeme, Maji na Uboreshaji wa Makazi

i. Wakala wa Nishati Vijijini ilipanga kusambaza umeme kwenye vijiji vya Tanzania Bara vinavyokadiriwa kufikia 12,268 kuanzia mwaka 2013 hadi kufikia mwaka 2021. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, mradi huo ulikuwa umefikisha umeme kwenye vijiji 4,395 sawa na asilimia 36 kwa kipindi cha miaka mitano. Hali hii inaondoa uwezekano wa kufikia lengo la kusambaza umeme kwenye vijiji 7,873 vilivyobaki katika kipindi cha miaka mitatu iliyosalia hadi kufikia mwaka 2021.

ii. Kulikuwa na kasi ndogo ya utoaji wa mikopo na mchakato mrefu wa manunuzi katika Mradi wa uboreshaji wa makazi ambao unatarajiwa kukamilika mnamo tarehe 28 Juni, 2019. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa kiasi kikubwa cha fedha cha shilingi bilioni 81.80 sawa na asilimia 60 ya fedha za mkopo zilizotolewa kwa ajili ya mradi huu. Hivyo, kuna uwezekano mdogo wa fedha hizi kutumika kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2019.

iii. Ukaguzi wa miradi ya maji ulibaini kuwa miradi ya maji 65 inayotekelezwa na Halmashauri 22 za Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye thamani ya shilingi bilioni 63.7 ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha kati ya miezi 3 hadi 48. Uchelewaji huu ulitokana na uwepo wa wakandarasi wasio na uwezo, ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini, changamoto za usanifu wa michoro na mapungufu yatokanayo na manunuzi.

Mapendekezo: Serikali iweke utaratibu wa uwajibikaji ili kuhakikisha fedha za miradi zinapelekwa kwa wakati na kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kutoathiri utekelezaji kwa ufanisi wa miradi hiyo.

7.4 Masuala ya Usimamizi wa Bajeti

i. Watekelezaji 14 wa miradi 2 walifanya matumizi ya takribani shilingi milioni 79.79 bila kutumia vifungu vilivyostahili kufanya matumizi hayo. Miradi hiyo ni HBF ambapo watekelezaji 11 walitumia shilingi milioni 67.73 na mradi wa WSDP watekelezaji 3 walitumia shilingi milioni 12.06. Kufanya malipo kwa kutumia vifungu visivyostahili kunaathiri utekelezaji wa shughuli za miradi zilizopangwa.

ii. Kiasi cha shilingi bilioni 2.03 kilitumika nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Watekelezaji 14 wa miradi miwili. Mradi wa HBF ulitumia shilingi milioni 84 na mradi wa WSDP ulitumia shilingi bilioni 1.95.

ii. Watekelezaji 203 wa miradi mitano hawakupokea shilingi bilioni 156.9 kutoka kwa washirika wa maendeleo. Miradi hiyo ni: ASDP shilingi bilioni 1.1 kwa watekelezaji 5, Sekta ya Elimu shilingi bilioni 18.1 kwa mtekelezaji 1, HBF shilingi bilioni 11.0 kwa watekelezaji 57, WSDP shilingi bilioni 124.3 kwa watekelezaji 133 na Sekta ya Maendeleo ya Jamii shilingi bilioni 2.4 kwa watekelezaji 7. Kutokupokelewa kwa fedha hizo kunakwamisha kufikiwa kwa malengo ya miradi iliyokusudiwa kutekelezwa.

iii. Malipo ya shilingi milioni 98.8 yalifanywa na watekelezaji 7 wa mradi wa HBF kinyume na matakwa ya Miongozo ya Mpango Kabambe wa Afya wa 2011.

Mapendekezo: Serikali iweke utaratibu wa uwajibikaji ili kuhakikisha fedha zinapelekwa kwa watekelezaji wa miradi kwa wakati uliopangwa na kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kutoathiri utekelezaji wa miradi kwa ufanisi.

7.5 Mapungufu katika Usimamizi wa Fedha

i. Malipo kiasi cha shilingi bilioni 16.6 yalifanywa na watekelezaji wa miradi 111 kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali bila uthibitisho wa stakabadhi za kielektroniki.

ii. Watekelezaji wa miradi 46 hawakukata kodi ya zuio kiasi cha shilingi milioni 190.1 hivyo Serikali ilikosa mapato kutokana na kodi ambayo haikukusanywa.

iii. Malipo ya kodi ya ongezeko la thamani kiasi cha shilingi bilioni 12.16 yalifanywa na watekelezaji wa miradi 45 kinyume na makubaliano ya mikataba ya utekelezaji wa miradi husika.

iv. Masurufu kiasi cha shilingi bilioni 1.08 kwa watekelezaji wa miradi 22 hayakurejeshwa siku 14 baada ya kumalizika kwa shughuli zilizokusudiwa. Hii ni kinyume na Agizo 40 (3) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kanuni 103(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001.

v. Nyaraka za malipo kiasi cha shilingi milioni 285.37 kwa watekelezaji wa miradi 16 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Hii iliathiri mawanda ya ukaguzi katika kujiridhisha uhalali wa malipo husika.

vi. Malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 38.53 kwa watekelezaji wa miradi 170 hayakuwa na nyaraka za kutosha. Hii ni kinyume na Agizo 8 (2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kanuni 95(4) ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001.

vii. Fedha za fidia kiasi cha shilingi bilioni 2.70 hazikulipwa kwa watu walioathirika na utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo ipo chini ya mradi wa Maendeleo wa Jiji la Dar es Salaam na Programu ya Kusaidia Miundombinu ya Sekta ya Usafirishaji Dar es Salaam.

viii. Fedha za wanufaika wa mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania ambazo hazikutumika kiasi cha shilingi milioni 451.49 zilichelewa kurudishwa kwenye akaunti kuu ya Mfuko na kuendelea kuwekwa kwenye akaunti za halmashauri kwa takribani siku saba. Hii ni kinyume na mwongozo wa mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania.

ix. Malipo kiasi cha shilingi bilioni 1.12 kwa watekelezaji wa miradi 45 yalifanyika kwa shughuli zisizokubaliwa kinyume na makubaliano ya mikataba ya miradi.

Mapendekezo: Maafisa Masuhuli waimarishe udhibiti wa ndani kwenye malipo,ukataji wa kodi ya zuio, utunzaji wa nyaraka na urejeshaji wa masurufu. Serikali itengeneze miongozo ambayo itawawezesha watekelezaji wa miradi kuomba misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani pamoja na kuzingatia makubaliano ya mikataba.

7.6 Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

i. Watekelezaji wa miradi 42 walifanya manunuzi ya bidhaa na huduma za thamani ya shilingi milioni 868.45 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila ushindani wa bei kutoka kwa angalau wazabuni watatu. Hii ni kinyume na Kanuni 76 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 na Jedwali la Kwanza la Kanuni Zinazoongoza Taratibu za Zabuni katika Halmashauri za Mwaka 2007.

ii. Watekelezaji wa miradi 17 katika Sekta ya Afya walishindwa kutoa ushahidi wa kupokea bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 8.95 zilizonunuliwa kutoka kwa wazabuni mbalimbali. Hii ni kinyume na Agizo 71(1) (b) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kanuni 114 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

iii. Vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.59 vilivyonunuliwa na watekelezaji wa miradi 57 bila ya kuviandikisha kwenye leja ya vifaa husika hivyo kuzuia ufuatiliaji wa utumikaji wa vifaa hivyo. Hii ni kinyume na Agizo 59(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

iv. Vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 559.22 vilinunuliwa na watekelezaji wa miradi 31 kwa wazabuni binafsi wa vifaa tiba bila idhini ya Bohari Kuu ya Dawa.

v. Watekelezaji wa miradi 13 walifanya manunuzi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.13 bila kuhakikiwa na kuidhinishwa na Kamati ya Mapokezi. Hii ni kinyume na Agizo 58(1-2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kanuni 245 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

vi. Watekelezaji wa miradi 25 walifanya manunuzi ya vifaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 2.75 kutoka kwa wazabuni mbalimbali bila kibali cha Bodi za Zabuni. Hii ni kinyume na Kanuni 57(3)(a) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

Mapendekezo: Maafisa Masuuli, Bodi za Zabuni na vitengo vya manunuzi vihakikishe manunuzi ya bidhaa na huduma yanafuata taratibu za manunuzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zake.

7.7 Udhibiti wa Kiutawala

i. Magari 31 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) yaliyopo kwa watekelezaji wa miradi 31 yamechakaa na kukaa kwa muda mrefu kwenye karakana bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa.

ii. Watekelezaji wa miradi 8 wana upungufu wa zahanati 109, vituo vya afya 32, nyumba za watumishi 63 na wodi 45.

iii. Halmashauri 314 zinazotekeleza miradi iliyo chini ya Programu ya maendeleo ya Sekta za Kilimo, Afya na Maji zina upungufu wa watumishi 48,710 ambao huathiri utendaji wa shughuli za miradi.

Mapendekezo: Maafisa Masuhuli wahakikishe kuwa magari yaliyochakaa yanafanyiwa matengenezo au kuuzwa ili yasiendelee kuchakaa zaidi. Vilevile Maafisa Masuhuli wawasiliane na mamlaka husika kuhakikisha kuwa tatizo la upungufu wa miundo mbinu pamoja na upungufu wa watumishi linapatiwa ufumbuzi.


!?
TRILIONI 382.6
MASHAURI YA KODI
TRA

SURA YA NANE

8.0 RIPOTI ZA UKAGUZI WA UFANISI

Sura hii inatoa taarifa ya kaguzi kumi na moja (11) za ufanisi zilizofanyika kwa mwaka unaoishia tarehe 31 Machi 2019. Madhumuni ya ukaguzi wa ufanisi ni kutoa tathmini ya kiwango ambacho thamani ya fedha yaani uwekevu, tija na ufanisi huzingatiwa na taasisi za serikali zinapotumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yake. Maeneo ya kufanya ukaguzi wa ufanisi hubainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali ikiwemo malalamiko kutoka kwa wananchi au umuhimu wa eneo husika kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka huu ripoti za kaguzi za ufanisi zilizowasilishwa bungeni ni kama ifuatavyo:

8.1 Usimamizi wa ujezi wa miundombinu ya Umwagiliaji

Lengo la ukaguzi:

Lengo la Ukaguzi huu lilikuwa kuangalia kama Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilisimamia ipasavyo shughuli za ujenzi wa miradi ya umwagiliaji kabla na wakati wa utekelezaji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji ulio endelevu kwa ajili ya umwagiliaji.

Mapungufu yaliyobainika

i. Usimamizi Usiojitosheleza wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika Hatua za Mipango na Utekelezaji Upembuzi yakinifu haukufanyika kama ilivyopangwa ndani ya kipindi cha miaka minne (2014/15 hadi 2017/18). Uchambuzi wa taarifa unaonesha kuwa pembuzi 11 tu ndiyo zilitekelezwa kati ya 360 zilizopangwa sawa na asilimia 3.

Vilevile, Upembuzi usio wa kina umepelekea kuacha baadhi ya vipengele muhimu ambavyo vimesababisha gharama za miradi kupanda kwa shilingi milioni 665.6.

ii. Kulikuwa na uchelewaji wa kukamilika kwa miradi ya umwagiliaji kwa kiwango cha asilimia 76 nje ya muda wa mkataba. Ilibainika kuwa kukosekana kwa mipango-kazi mahususi ya ujenzi ilikuwa ni sababu kuu ya miradi mingi kuchelewa kukamilika.

Mapendekezo : Wizara ya kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ianzishe kanzi data itakayokuwa ikihifadhi taarifa za idadi ya miradi ya umwagiliaji, hali ya maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo kifedha na kiujenzi ili isaidie upangaji, usimamizi na ufuatiliaji.

8.2 Ukaguzi wa Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini

Lengo la ukaguzi

Ukaguzi wa Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini ulilenga kuangalia kiwango ambacho Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kinahakikisha upatikanaji wa Maji Safi Vijijini.

Mapungufu yaliyobainika

i. Miundombinu ya maji iliyojengwa vijijini ina uwezo wa kusambaza maji kwa asilimia 85.2 ya mahitaji ya watu vijijini wakati kiasi cha watu wanaopata maji ni asilimia 58.7 tu kutokana na baadhi ya miradi iliyojengwa kutofanya kazi.

ii. Asilimia 79 ya miradi 58 iliyokaguliwa haikukamilika kwa wakati kwa sababu mbalimbali ikiwemo ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, uwezo mdogo wa kifedha na kiufundi wa wakandarasi, na usimamizi duni wa Wizara ya Maji na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

iii. Theluthi moja (1/3) ya miradi ya maji iliyotekelezwa katika mikoa sita iliyotembelewa ilikuwa na ongezeko la gharama kwa kati ya shilingi bilioni 1.2 na shilingi bilioni 7.1. Hii ilisababishwa na udhaifu katika usanifu wa michoro ya miradi, uandaaji wa nukuu za ukubwa wa kazi na uchambuzi hafifu wa mahitaji ya miradi husika.

Mapendekezo: Wizara ya maji inatakiwa kuhakikisha kuwa wanapima maji kabla ya kuanza kutumia, wanafanya upembuzi yakinifu kwa miradi ya maji iliyopangwa kutekelezwa, wanapitia usanifu na mikataba ya miradi ya maji, utafutaji wa maji chini ya Ardhi unafanywa na watu wenye uzoefu, kunakuwa na pesa za uhakika na maalum kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji, usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya maji unaimarishwa kwenye ngazi ya halmashauri hadi wizara.

8.3 Ukaguzi wa usimamizi wa Miradi ya Maji ya Visima Virefu

Lengo la Ukaguzi:
Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Maji inasimamia kwa ufanisi Miradi ya Maji ya Visima Virefu.

Mapungufu yaliyobainika

i. Kati ya visima 1,485 vilivyochimbwa, visima 490 sawa na asilimia 33 havikutoa maji. Jumla ya shilingi milioni 764 zilitumika katika miradi ya maji ya visima virefu ambavyo havikutoa maji.

ii. Jumla ya sampuli 709 kati ya 6,615 za maji zilizofanyiwa uchunguzi hazikukidhi viwango vya ubora kwa matumizi ya binadamu. Kulikuwa na viashiria vikubwa vya kutokuwepo kwa ubora wa maji kama vile uwepo wa kiwango kikubwa cha mangenisi, floridi, alkali, uchafu na vimelea vya magonjwa. Hii imetokana na kutokuwepo kwa utafiti wa kutosha wa maji ya ardhini kwa nchi nzima.

iii. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (8) nane zilizotembelewa, miradi ilichelewa kwa asilimia 50 wakati mradi mmoja ulichelewa kwa asilimia 78 ya muda wa ujenzi uliokadiriwa. Hali hii ilitokana na uwezo mdogo wa kiufundi na kifedha wa wakandarasi, kuchelewa kwa fedha za miradi kutoka Serikalini na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi.

Mapendekezo: Wizara ya Maji ifanye utafiti na kuhifadhi kumbukumbu ya uwepo na upatikanaji wa maji ya chini ya ardhi nchini. Vilevile, iwapatie matokeo ya utafiti huo watekelezaji wote muhimu wa miradi ya visima vya maji.

8.4 Ukaguzi wa usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura katika Hospitali za Rufaa za Ngazi ya Juu

Lengo la Ukaguzi:

Lengo la ukaguzi ilikuwa ni kuangalia iwapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto ina mfumo madhubuti wa kuhakikisha ufanisi wa usimamizi wa utoaji Huduma za Afya za Rufaa na Dharura katika Hospitali za Rufaa na Ngazi za Juu.

Mapungufu yaliyobainika

i. Idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika Hospitali za Rufaa na Ngazi za Juu

inazidi uwezo wa hospitali husika kutokana na kupandishwa daraja kutoka Hospitali zinazotoa huduma za afya ya msingi kwenda daraja la juu pasipo kuzingatia miundombinu iliyopo, pamoja na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika hospitali hizo na upatikanaji wa madaktari bingwa.

ii. Huduma za Afya za Rufaa zitolewazo katika Hospitali za Rufaa Ngazi ya Juu hazijitoshelezi. Wizara ya Afya haijaanzisha kiwango stahiki cha muda ambao wagonjwa wanapaswa kusubiri kabla ya kupata huduma ya afya. Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya wagonjwa wenye rufaa na dharura husubiri kwa wastani wa saa 3 hadi 4 kabla ya kupata huduma.

iii. Hospitali sita (6) kati ya saba (7) za Rufaa za Mkoa zilizokaguliwa hazikuwa zikitoa huduma zote za afya kama inavyostahili kutolewa na Hospitali ya Rufaa ikiwa ni pamoja na tiba za Magonjwa ya Kawaida, Huduma za Afya ya Watoto, Uzazi na Ujauzito, Kinywa na Meno na Upasuaji.

iv. Wizara ya Afya haijafuatilia na kutathmini utendaji wa Hospitali za Rufaa katika utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura. Hii imesababishwa na kutokuwepo kwa mipango ya ufuatiliaji na kuainisha viashiria katika kufuatilia utendaji wa Hospitali za Rufaa.

Mapendekezo: Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iweke mikakati ya kuhakikisha hospitali za rufaa zina uwezo wa kutoa huduma za dharura na huduma za msingi za rufaa. Pia Wizara iandae na kusambaza miongozo ya kitaifa ya rufaa na kuhakikisha usawa katika ugawaji wa rasilimali kulingana na mahitaji katika ngazi mbalimbali za hospitali za rufaa.

8.5 Ukaguzi wa usimamizi wa Ujenzi wa Majengo Mijini Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini endapo Ofisi ya Rais- TAMISEMI, kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa inafuatilia kikamilifu shughuli za Ujenzi wa majengo ya mijini ili kuhakikisha majengo yote yanayojengwa yanazingatia viwango vinavyotakiwa na kwamba ni salama kwa matumizi.

Mapungufu yaliyobainika

i. Kuwepo kwa majengo katika maeneo yasiyopangwa na makazi yasiyo rasmi. Maeneo hayo yamekuwa na nyumba zenye ubora hafifu, zilizojengwa bila uwepo wa upatikanaji wa huduma muhimu kama vile barabara, mitaro ya maji ya mvua, huduma za maji safi, pamoja na huduma zingine za dharura.

ii. Kulikuwa na uchelewashaji wa vibali vya ujenzi kati ya mwezi mmoja hadi miaka miwili kuanzia pale maombi yalipowasilishwa na kibali kinapoidhinishwa. Mamlaka za serikali za mitaa hazikuwa na mifumo ya usajili ya maombi ya vibali vya ujenzi pamoja na utoaji wa elimu kwa umma juu ya mchakato na umuhimu wa vibali vya ujenzi.

iii. Mamlaka za serikali za mitaa hazikuwa na mikakati, mipango, miongozo mahususi ya ukaguzi wa shughuli za ujenzi wa majengo na bajeti za kufuatilia shughuli za majengo katika maeneo yao. Hapakuwa na kanzidata inayoonesha idadi na taarifa za majengo yanayoendelea kujengwa au kukamilika.

iv. Hakuna mawasiliano ya kueleweka kati ya Taasisi muhimu kama vile Wakala wa Majengo Tanzania; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kupanga na kutekeleza shughuli za ujenzi wa nyumba mijini.

Mapendekezo: TAMISEMI inapaswa kuanzisha mikakati na mifumo ambayo itahakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamia kwa ufanisi utoaji wa vibali vya ujenzi kwa kuzingatia muda uliotolewa.

8.6 Ukaguzi wa matengenezo ya Mitambo ya kuzalisha Umeme

Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi huu lilikua ni kutathmini kama TANESCO inafanya matengenezo ya mitambo yake ya kuzalisha umeme kwa kuzingatia viashiria hatarishi (vihatarishi).

Mapungufu yaliyobainika

i. Kuwepo kwa utafiti hafifu kuhusu bei halisi za vipuri vya mitambo. Hali hii ilisababisha baadhi ya vipuri kuwa juu ya bajeti kwa kiwango cha hadi asilimia 99 wakati baadhi ya vipuri vilikuwa na bajeti pungufu kwa kiwango cha hadi asilimia 116.

ii. Kutokuwepo kwa wataalamu maalumu na watengenezaji wa mitambo walioidhinishwa kufanya matengenezo. Hivyo, TANESCO inategemea wataalamu kutoka nje ya nchi kufanya matengenezo ya mitambo. Mapungufu haya yalionekana zaidi katika mitambo ya kuzalisha umeme wa gesi. TANESCO ilishindwa kupeleka wafanyakazi wake kujifunza kutoka kwa watengenezaji wa mitambo ili kupata ujuzi mahsusi.

iii. Kutofanyika kwa matengenezo yanayozingatia viashiria hatarishi ili kuweka vipaumbele katika udhibiti wa viashiria hivyo.

Hali hii inaweza kusababisha nchi kukosa umeme wa uhakika na kushindwa kufikia malengo katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

Mapendekezo: Wizara ya Nishati inapaswa kuhakikisha kuwa inapokea taarifa za matengenezo na hali ya mitambo ya kufua umeme kisha kutoa maelekezo.

TANESCO inapaswa kuhakikisha kuwa mchakato wa manunuzi unafanyika kwa kufuata tararibu na sheria zilizopo kwa wakati na mipango ya mwaka ya manunuzi itekelezwe mapema pindi tu bajeti inapopitishwa.

8.7 Ukaguzi wa ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa Pamoja

Lengo la Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa Pamoja unafanya kazi kwa kuzingatia gharama, muda, idadi, na viwango vya ubora wa magari.

Mapungufu yaliyobainika

i. Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) haukuendesha ushindani madhubuti katika kufanya manunuzi ya magari ya Serikali.

ii. Bei iliyotolewa na Kampuni ya Toyota Tanzania ilikuwa juu kwa asilimia 15 hadi 49 ikilinganishwa na bei za magari za Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa aina ya magari na viwango vya ubora vinavyofanana. Ilibainika kuwa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini ukinunua magari ya viwango vya ubora vinavyofanana kutoka kwa mawakala wengine tofauti na Shirika la Maendeleo

la Umoja wa Mataifa, hupoteza takribani shilingi milioni 10 hadi 50 kwa kila gari moja lililonunuliwa.

iii. Ukaguzi ulibaini kuwa magari yaliyonunuliwa hayakufika kwa wakati wala kwa idadi iliyotakiwa. Ucheleweshaji wa magari ulifikia hadi siku 130.

iv. Taasisi nunuzi ziliwasilisha mahitaji yao ya magari kwa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini kwa wakati. Hata hivyo, Wakala umekuwa ukiagiza magari kulingana na mahitaji yaliyoletwa na Taasisi nunuzi mojamoja badala ya kukusanya maombi hayo na kufanya manunuzi kwa pamoja jambo linaloiongezea gharama Serikali.

Mapendekezo : GPSA waweke mpango mkakati sambamba na viashiria vya utendaji.Viashiria hivyo viweze kupimika kwa muda mfupi na mrefu.Vile vile viashiria hivyo viweze kuelezea malengo ya ununuzi wa pamoja kwa kungalia zaidi gharama za ununuzi,muda wa upatikanaji wa magari kwa Taasisi nunuzi na viwango vinavyokidhi matumizi yaliyotarajiwa na mnunuzi. Wizara ya Fedha na Mipango iimarishe namna ya kuisimamia GPSA ili kuhakikisha kwamba ununuzi wa magari kwa pamoja unakuwa na tija kwa serikali.

8.8 Ukaguzi wa usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Lengo ya Ukaguzi:

Lengo la ukaguzi lilikua ni kutathmini, ni kwa kiwango gani Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI zimeandaa mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mapungufu yaliyobainika

i. Kuna upungufu wa asilimia 68 wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia ikiwemo mashine za kurudufisha na kuchapisha maandishi ya nuktanundu, shime-sikio, vifaa vya kupima kiwango cha usikivu na visaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona na ulemavu wa akili.

ii. Kuna upungufu wa walimu wa elimu maalum kwa ngazi ya shule ya msingi kwa takribani asilimia 44. Walimu wa elimu maalum waliopo ni 2460 kati ya walimu 4428 wanaohitajika nchini.

iii. Kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, walimu 952 kati ya 2460 sawa na asilimia 39 ya walimu wa elimu maalum hawakupatiwa mafunzo ya muda mfupi. Kadhalika, kwa kipindi cha miaka minne iliyopita asilimia 61 ya walimu wa elimu maalum hawakupata mafunzo ya muda mfupi kwenye eneo la elimu maalum. Hii inatokana na kuwepo kwa chuo kimoja tu kwa ajili ya mafunzo ya Elimu Maalum.

iv. Wizara ya Elimu haijaandaa utaratibu wa namna ambayo wanafunzi wenye ulemavu wa kuona watafanya mitihani ya hesabu na sayansi. Hii ni kinyume na Kanuni 29(3) ya Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016.

Mapendekezo: Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais-TAMISEMI zinatakiwa kuhakikisha wanaweka kipaumbele katika mipango yao ili kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

8.9 Ukaguzi wa usimamizi wa Utoaji wa huduma za Bima ya Afya zinazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Lengo la Ukaguzi:

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Afya, na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unatekeleza kikamilifu majukumu yao ya usimamizi wa utoaji wa huduma za bima ya afya nchini.

Mapungufu yaliyobainika

i. Hadi kufikia mwezi Juni 2018, ni asilimia 32 tu ya Watanzania ndiyo walikuwa wanatumia bima ya afya. Idadi hii inajumuisha wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ambao ni asilimia 25 na wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

ii. Kumekuwepo na matumizi yaliyozidi kiwango cha uchangiaji wa wanachama katika makundi mbalimbali ya wanachama wa Mfuko. Kwa mfano, kundi la KIKOA matumizi yalikuwa asilimia 710; kundi la viongozi wa dini matumizi yalikuwa asilimia 401; kundi la Toto Afya Kadi matumizi yalikuwa asilimia 298; kundi la madaktari wa mafunzo kwa vitendo matumizi yalikuwa asilimia 174; kundi la wanafunzi matumizi yalikuwa asilimia 171; na kundi la wachangiaji binafsi matumizi yalikuwa asilimia 160. Hali hii isipodhibitiwa, itadhohofisha hali ya kifedha na utendaji wa Mfuko.

iii. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulitoa mkopo wa shilingi bilioni 24.6 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani mwezi Agosti 2010 kwa ajili ya ununuzi wa magari ambapo wizara ilitakiwa kuanza kurejesha mkopo huo baada ya kipindi cha mwaka mmoja yaani Agosti 2011, kwa kipindi cha miaka nane. Hadi kipindi cha ukaguzi huu, mkopo huo ulikuwa bado haujarejeshwa.

iv. Mwaka 2012, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulitoa kiasi cha shilingi bilioni 114.1 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa bila ya kuwa na makubaliano yoyote ya kimaandishi. Hali hii ilisababisha kutolipwa kiasi chochote hadi kipindi cha ukaguzi huu.

Mapendekezo: Kuimarisha mifumo itakayowezesha kuongezeka kwa idadi ya wanachama wachangiaji wa kundi la hiari kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Kufanya utafiti thabiti kabla ya kuanzishwa kwa makundi mbalimbali ya wanachama wapya ili kupunguza athari za kutofikia malengo na kuanzisha mikakati itakayohakikisha kunakuwa na ufanisi kwenye urejeshaji wa mikopo iliyotolewa.Pia kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na ufanyaji tathmini utakaojumuisha viashiria muhimu vya kiutendaji kwa malengo ya kupima utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

8.10 Taarifa ya Ufanisi ya Upatikanaji na Usambazaji wa Pembejeo bora za Kilimo

Lengo la Ukaguzi:

Lengo la ukaguzi huu ilikua kupima kama Wizara ya kilimo Kupitia Taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu nchini na Mamlaka ya Udhibiti ubora wa Mbolea wanahakikisha uwepo wa pembejeo bora kwa wakulima ili kukuza uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini.

Mapungufu yaliyobainika

i. Wizara ya Kilimo haitekelezi kiufanisi hatua za kutambua mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo ili kuhakikisha upatikanaji wake kwa wakulima. Takwimu zinaonesha kuwa, kwa kipindi cha miaka 4 iliyopita, wastani wa usambazaji wa pembejeo za kilimo ulikuwa asilimia 39 tu ya mahitaji.

Hii ilisababishwa na Wizara ya Kilimo kukadiria mahitaji ya pembejeo kwa kutumia taarifa za miaka iliyopita ambazo si za kuaminika.

ii. Mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima haufanyi kazi vizuri katika kuhakikisha kuwa usambazaji unafanyika kwa wakati. Kulikuwa na ucheleweshaji wa pembejeo kwa kipindi cha kati ya miezi mitatu (3) hadi mitano (5). Ucheleweshaji huu ulitokana na Wizara ya Kilimo kuchelewa kusambaza vocha za kununulia pembejeo.

iii. Uwepo wa mbegu za mahindi ambazo hazikuwa na uwezo wa kuota, kwa mfano Pioneer 2859 na DKC 90-89. Aidha, kulikuwa na usambazaji wa mbegu ambazo zinaota lakini hazitoi mazao kama ilivyotarajiwa mfano Pioneer 3253 and SC 625. Pia, ukaguzi ulibaini uwepo wa zaidi ya asilimia 50 ya wauzaji wa pembejeo ambao hawakusajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu vya Kitropiki, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania.

iv. Kumekuwa na usajili hafifu wa mbolea na mbegu unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu. Hali hii ilidhihirishwa na uwepo wa mbegu na mbolea zisizosajiliwa ambazo zilikuwa zinatumiwa na wakulima na kusababisha malalamiko ya ubora wa mbegu na mbolea hizo.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe inaimarisha mifumo ya kuhakikisha ubora wa pembejeo za kilimo zinazosambazwa nchini ikiwa ni pamoja na kuweka mbinu za kupima ufanisi ambazo zitasaidia katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera hususani ubora wa pembejeo za kilimo.

Pia Serikali ihakikishe inatenga maeneo yatakayotumika kuzalishia pembejeo bora kwa wakulima.

8.11 Ripoti ya Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ripoti Tano za ufanisi zilizofikishwa Bungeni Mwaka 2015

Lengo la Ukaguzi:
Lengo la ukaguzi huu ni kufanya tathmini ya kiwango ambacho Taasisi kaguliwa zimetekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ripoti za mwaka 2015.

Mapungufu yaliyobainika

i. Kati ya mapendekezo 85 yaliyotolewa, ni asilimia 26 tu ambayo ni sawa na mapendekezo 22 ndiyo yaliyotekelezwa kikamilifu; asilimia 48 yalitekelezwa kwa kiasi; asilimia 26 hayakutekelezwa kabisa.

ii. Taasisi zote Nane (8) ambazo zilipewa mapendekezo ya ukaguzi hazikuwa na mfumo madhubuti wa utawala ambao una mgawanyo sahihi wa majukumu na mpangilio wa utoaji taarifa. Pia Taasisi hizo hazina mfumo wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za ufanisi yaliyotolewa kwa Taasisi hizo.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe kwamba Wizara zote, Idara, Mashirika pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za ufanisi.

TATHMINI INAONYESHA KASI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI IMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 8.2
TUNAKOELEKEA NI KUZURI ZAIDI

SURA YA TISA

9.0 RIPOTI YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Taarifa hii inatoa muhtasari na majumuisho ya matokeo ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA

Ukaguzi huu ulijikita katika mifumo mikubwa mitatu. Mifumo hiyo ni; Mfumo wa usimamizi wa fedha za Umma kwenye Serikali za Mitaa (IFMS Epicor) katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu serikalini (Lawson) katika ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mfumo wa Serikali wa malipo ya kielektroniki (GePG) katika wizara ya Fedha na Mipango. Pia inajumuisha mifumo ya udhibiti wa ndani ya TEHAMA kwa Mashirika ya Umma na Wizara pamoja na ukaguzi wa usimamizi wa miradi ya TEHAMA. Kaguzi zilizofanyika na mapungufu yaliyobainika ni kama ifuatavyo:

9.1 Ufanisi wa mifumo ya TEHAMA

Mifumo ya Ankara isiyompunguzia mwananchi usumbufu katika kufanya malipo

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa usumbufu kwa wateja unaohusiana na kutopatikana mara kwa mara kwa mifumo, kushindwa kutoa ankara kwa mteja, ugumu wa kupata nambari ya udhibiti (control number), mifumo kutoweza kutoa nambari moja ya udhibiti kwa malipo mengi ya pamoja na utaratibu usio na ufanisi wa kushughulikia malalamiko ya wateja. Hii imesababisha mapato kutokusanywa kwa wakati na wakati mwingine kutokusanywa kabisa, pia inaondoa uaminifu kwa wateja na wananchi juu ya ubora na ufanisi wa mfumo wa malipo wa serikali (GePG).

Mapendekezo: Serikali ihakikishe mifumo ya Ankara na taratibu za malipo ya serikali inakuwa rahisi kwa mlipaji na inapatikana wakati wote ili kuepusha usumbufu kwa Wananchi.

9.2 Udhaifu wa Mifumo ya TEHAMA kutokuwa funganishi

i. Katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa Mfumo wa usimamizi wa fedha za Umma (Epicor) haujaunganishwa moja kwa moja na mfumo wa malipo makubwa na ya haraka unaoendeshwa na Benki Kuu ya Tanzania (TISS) ambapo inaweza kusababisha hatari ya malipo kufanyika zaidi ya mara moja pasipo kubainika.

ii. Katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa Mfumo wa usimamizi wa fedha za Umma (Epicor) haujafungamanishwa na mfumo wa Akaunti ya pamoja ya Hazina. Hivyo, katika mapitio ya uhamishaji wa fedha za serikali za mitaa kutoka benki za biashara kwenda Benki Kuu ya Tanzania yamebainika mapungufu ya udhibiti katika kuhakikisha kuwa kiasi cha fedha kinachoonekana kwenye mfumo wa Epicor kinalingana na kiasi halisi cha fedha kilichotumwa kutoka benki za biashara kwenda Benki Kuu ya Tanzania.

iii. Mfumo shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara wa usimamizi wa rasilimali watu (Lawson) haujafungamanishwa na Mfumo wa usimamizi wa fedha za umma (Epicor) pamoja na mfumo wa ajira (Ajira portal). Hivyo, imesababisha kuwepo kwa matukio ya kugushi barua za uajiri kutoka Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwenda kwa waajiri ambapo inaweza kupelekea kuwepo kwa ama waajiriwa hewa katika mfumo wa taarifa za kiutumishi na Mishahara. Aidha, kama mifumo hii mitatu ingekuwa imefungamanishwa ingeweza kuondoa tatizo hilo, kwa sababu mfumo wa Ajira ulianzishwa kusimamia mchakato wa kuajili kutoka hatua ya maombi ya kazi, usaili na uajiri. Mfumo huu wa ajira una

uwezo wa kutengeneza namba ya utambulisho ya kipekee kwa mtu anayeajiriwa ambayo inatumika kama namba ya mwajiriwa mpya kwenye mfumo wa Lawson. Vile vile, Mfumo wa Epicor kutounganishwa na Mfumo wa Lawson imesababisha kutengeneza bajeti ya rasilimali watu nje ya mfumo wa Lawson. hii, inaweza kusababisha kufanya matumizi ya fedha kwenye rasilimali watu zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

iv. Ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA ulibaini kuwa, Mifumo mingi ya kiuhasibu na mifumo ya makusanyo ya mapato haijafungamanishwa. Ukaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwenye mfumo wa utoaji wa leseni yaabi "License and Order (LOIS)", Ukaguzi wa Mamlaka ya Maji Safi na majitaka Dar es Salaam (DAWASCO) kwenye mfumo wa "Engineering Design Analysis Management (EDAMS)" na ukaguzi wa Wakala wa Mabasi yaendayo haraka (DART) kwenye mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani umebaini kuwa mifumo hiyo haijaunganishwa na mifumo ya kiuhasibu ya Taasisi hizo. Hivyo, taarifa za mapato yaliyokusanywa yanaingizwa kwenye mfumo wa kiuhasibu na mtumiaji mfumo ambapo inaweza kutokea makosa ya kutoingiza taarifa sahihi na kusababisha kutokufautiana kwa taarifa zilizo kwenye mfumo wa mapato na mfumo wa uhasibu.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe mifumo inakuwa funganishi kuongeza ufanisi, uthibiti wa ndani, kupunguza gharama za usimamizi na kuzuia upotevu wa mapato.

9.3 Utendaji wa mifumo ya TEHAMA

Kuwepo kwa mgawanyo hafifu wa majukumu ambayo hayatakiwi kufanywa na mtu mmoja kwenye mifumo

i. Tathmini ya mfumo wa Epicor katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibaini kuwepo kwa mapungufu katika mgawanyo wa majukumu yasiyotakiwa kufanywa na mtu mmoja. Aidha, ilibainika kuwa waweka hazina wa wilaya na halmashauri mbalimbali wana uwezo wa kuingiza taarifa za bajeti, kufanya mgawanyo wa fedha, kuanzisha malipo, kuandaa hati za malipo na kuidhinisha malipo hayo. Majukumu haya yakifanywa na mtu mmoja yanaweza kupelekea ubadhirifu wa fedha kwa kuwa udhibiti kwenye mgawanyo wa majukumu ndani ya mfumo ni dhaifu.

ii. Mfumo wa kiuhasibu katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hauna udhibiti wa kumzuia mtumiaji kuidhinisha miamala ya kifedha ambayo ameianzisha mwenyewe. Kati ya hati 44,280 za malipo ambazo zilitengenezwa kutoka kwenye mfumo wa malipo ya kieletroniki wa TBS, hati 192 zilianzishwa, kuthibitishwa na kuidhinishwa na mtu mmoja.

iii. Katika mapitio ya mfumo wa Usajili na utoaji Leseni (SURLIS) wa Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Ardhi na Majini (SUMATRA) ilibainika kuwa hatua zote tatu za kutoa leseni zinafanywa na mtu mmoja ambaye ana uwezo wa kuingiza taarifa za magari, kuthibitisha taarifa hizo, kuidhinisha na kutoa hati za madai.

iv. Katika mapitio ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa (MIS) pamoja na vyeti vya usajili wa bidhaa za Chakula na Dawa katika Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ilibainika kuwa kati ya maombi 2,782 yaliyopokelewa, maombi 286 yalifanyiwa tathmini, kukaguliwa na kuidhinishwa na mtu mmoja.

v. Mapitio ya mfumo wa malipo ya kielektroniki Serikalini (GePG) yalibainisha kuwa mtumiaji wa mfumo wa Ankara mwenye jukumu la meneja ana uwezo

wa kuweka tarehe ya ukomo wa malipo ya ankara bila kuidhinishwa ambapo inaweza kupelekea mazingira ya udangayifu. Pia ilibainika kuwa meneja anaweza kutengeneza ankara ya malipo na kupata namba ya kumbukumbu ya malipo kutoka kwenye mfumo. Hivyo, mfumo hauna hatua ya ziada ya kuidhinishwa kwa ankara, hali hii inaweza kusababisha meneja kukadiria kiasi cha chini ukilinganisha na kiwango halisi kinachotakiwa kulipwa.

Mapendekezo: Serikali kupitia Taasisi husika ihakikishe kuwa, kunakuwepo na mgawanyo wa majukumu katika mifumo ya kifedha na Ankara wakati wa usanifu na utekelezaji wa mifumo.

Udhibiti kwenye mifumo usiozingatia miongozo na sera

i. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa Watumishi wenye namba ya utambulisho (cheki namba) zaidi ya moja kwenye mfumo wa rasilimali watu. Ukaguzi huo wa Mfumo wa rasilimali watu unaotumika na Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa umma katika kusimamia rasilimali watu serikalini ulibaini kuwa mfumo unatumia majina matatu ya mtumishi na tarehe yake ya kuzaliwa katika kutambua kama taarifa za mtumishi zipo tayari kwenye mfumo. Kila mtumishi aliyesajiliwa katika mfumo shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara ana cheki namba ya kipekee kama nambari ya utambulisho isiyofanana na mtumishi mwingine. Mapitio ya majina ya watumishi waliosajiliwa kwenye mfumo ulibaini watumishi 31 wenye cheki namba mbili tofauti. Hivyo inaweza kupelekea uwepo wa watumishi hewa kutokana na udhibiti wa kutumia majina matatu na tarehe ya kuzaliwa kuwa na mapungufu.

ii. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa Watumishi wenye makato yanayozidi theluthi (1/3) ya mshahara. Kulingana na muongozo namba 3 aya namba 8.5 wa Ofisi ya

Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma wa mwaka 2011 unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuhuli wakati wa kuidhinisha mikopo ya watumishi kuhakikisha kuwa, mtumishi mkopaji baada ya makato kwanye mkopo anabaki na kiasi ambacho si chini ya 1/3 ya mshahara wake wa jumla. Aidha, ilibainika kuwepo kwa watumishi 16,787 kati ya 526,498 ambao wana mishahara chini ya 1/3 japokuwa mfumo umesanifiwa kuzuia hili lisitokee.

iii. Udhibiti hafifu wa bajeti katika mfumo wa kihasibu wa serikali za mitaa, ilibainika kuwa matumizi ndani ya mfumo yalikuwa yanafanywa nje ya bajeti iliyoidhinishwa, vifungu vya bajeti vilikuwa na bakaa hasi yaani vilitumia fedha zaidi ya kiasi kilichopangwa kwenye bajeti na kitabu cha hesabu kina bakaa hasi kwa akaunti za leja.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe mapungufu yanafanyiwa kazi kwa kuhakikisha mifumo inasanifiwa na kufanya kazi kulingana na miongozo na sera zinavyoelekeza.

9.4 Taratibu zisizofanyika ndani ya mifumo

i. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa Maafisa Masuhuli wanaoidhinisha maombi ya malipo nje ya mfumo. Mapitio ya mifumo ya kiuhasibu na mifumo inayoendesha kazi za Serikali Kuu, Serikali za mitaa na Mashirika ya Umma imeonesha kuwa Maafisa masuhuli wanaidhinisha nyaraka zilizochapishwa nje ya mfumo, badala ya kuidhinisha nyaraka ndani ya mfumo husika. Hii imesababishwa na mifumo kutosanifiwa kuwawezesha Maafisa Masuhuli kuingia kwenye mfumo na kuidhinisha badala yake Maafisa wa chini wanaingiza taarifa kwenye mfumo ambazo zimeshaidhinishwa na maafisa masuhuli kwenye nyaraka.

ii. Ukaguzi ulibaini kuwa bidhaa na mizigo inayopita nchini kwenda nchi nyingine

hupita bila kuhakikiwa kwenye mfumo wa Forodha wa kuingiza na kuondosha mizigo kwa njia Kielectroniki (TANCIS) katika Mamalaka ya Mapato Tanzania (TRA). Mapitio ya taarifa za TANCIS juu ya bidhaa zinazosafirishwa kupitia mipaka ya Kabanga, Rusumo, Mutukula, Tunduma na Kasumulu yalibaini kuwa miamala 599 ya bidhaa zilipita nchini kwenda nchi nyingine pasipo kuhakikiwa kwenye mfumo wa TANCIS.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe Maafisa Masuhuli wanatumia mifumo na kuidhinisha maombi na miamala ndani ya mifumo. Aidha kuhakikisha mfumo wa TANCIS unatumika ipasavyo hasa kwa mizigo ambayo inapita ndani ya nchi kwenda nchi jirani ili Serikali iweze kupata mapato stahiki.

9.5 Kutokuwepo kwa utaratibu kwa serikali kujiridhisha juu ya miamala ya fedha

i. Kutohakikiwa kwa mapato ya UDART kupitia kadi za malipo za kielektroniki. Ukaguzi katika mfumo wa makusanyo ya mapato ya nauli za basi za UDART umebaini kuwa wahasibu wa DART wanauwezo wa kuona dashibodi ya mfumo tu, ambao unatumika kukusanya mapato ya nauli za basi kwa njia ya kielektroniki. Hivyo dashibodi inaweza kurekebishwa ili kuonyesha kile ambacho UDART anataka DART akione. Hivyo kuondoa uwezekano wa DART kufahamu mapato halisi yanayokusanywa na yanayoonyeshwa kwenye dashibodi.

ii. Ufuatiliaji hafifu wa makato ya asilimia 1.1 kwa watoa huduma wa simu za mkononi kutoka kwa malipo ya GePG. Serikali kupitia Wizara ya fedha iliingia mkataba na watoa huduma wa simu za mkononi kuwezesha mfungamano na GePG kwa makato ya asilimia 1.1 ambayo itatozwa kwa kila malipo yanayofanywa na mteja. Wizara ya Fedha hufanya ukaguzi wa kushtukiza ili

kufuatilia utekelezaji wa makato hayo. Utaratibu huu sio fanisi na toshelezi hivyo inaweza kusababisha watoa huduma za simu kuongeza kiwango cha makato zaidi ya asilimia ya makubaliano ambayo itaumiza walipaji wa malipo ya serikali.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe DART iwe na mfumo wake yenyewe wa kukusanya nauli na kuusimamia vilevile mtoa huduma (UDART) atumie mfumo huo. Pia Serikali iweke utaratibu madhubuti wa kuhakikisha gharama ambazo makampuni ya simu yanatoza kwa kila muamala wa malipo kwa njia ya GePG yanatozwa kulingana na mkataba.

9.6 Usimamizi wa mifumo na miradi ya TEHAMA

Kuwepo kwa mifumo tofauti ya TEHAMA inayofanya kazi moja

Mapitio ya mifumo ya TEHAMA katika taasisi za Serikali ilibaini kuwa ipo mifumo tofauti ambayo inafanya kazi moja. Baadhi ya mifumo hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mfumo	Taasisi	Kazi ya mfumo
Lawson	Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	Kusimama na kuhakiki taarifa za mishahara ya wafanyakazi.
GSPP	Wizara ya Fedha na Mipango	
National Business Portal	Wizara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara na BRELLA	Usajili na utoaji leseni za biashara “Daraja B”
LGRCIS	Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	
Salary Slip Portal	Wizara ya Fedha na Mipango	Kutoa “salary slip”
Watumishi Portal	Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora	

Mapendekezo: Serikali ihakikishe kunakuwepo na uratibu wa pamoja katika uanzishwaji na usimamizi wa miradi ya TEHAMA**.**

9.7 Matumizi hafifu ya moduli za mifumo ya TEHAMA

i. Ukaguzi ulibaini kutotumika kwa moduli ya manunuzi katika mfumo wa kihasibu (Epicor) wa Serikali za Mitaa. Mfumo huu una moduli ya manunuzi ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kusimamia utaratibu mzima wa manunuzi. Kutotumika kwa moduli hii kunapunguza ufanisi na kuongeza ugumu wa utunzaji wa taarifa za manunuzi.

ii. Kutotumika kwa moduli ya utunzaji na usimamizi wa taarifa za mali za kudumu katika mfumo wa kihasibu (Epicor) wa Serikali za Mitaa. Mfumo huu una moduli ya kutunza taarifa za mali za kudumu. Ukaguzi ulibaini kuwa moduli hii haitumiki na Mamlaka za Serikali za Mitaa nakupelekea taarifa za mali za kudumu kuhifadhiwa nje ya mfumo hivyo kuondoa ufanisi katika usimamizi wa mali za kudumu.

iii. Kutotumika kwa Moduli mbili kati ya tano za mfumo wa EDAMS wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es salaam (DAWASCO). Ukaguzi wa mfumo wa "Engineering Design Analysis Management System (EDAMS)" unaotumika na Mamlaka, ulibaini kuwa mfumo una moduli tano ambapo kati ya hizo, moduli mbili hazitumiki. Kutotumika kwa moduli hizi kunasababishwa na kutoingizwa kwa taarifa kamili za mtandao wa mabomba kwenye mfumo ambazo zinatumika na hizo moduli mbili. Aidha hakuna mpango mkakati unaoonyesha namna gani na lini taarifa za mtandao wa mabomba zitaingizwa kwenye mfumo japokuwa kulikuwa na timu iliyoundwa kwa ajili ya zoezi hilo.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe Ofisi ya Rais TAMISEMI na DAWASCO zinatumia moduli zote za mifumo ili kuongeza ufanisi na kuleta thamani ya fedha kwa Serikali kunufaika na moduli hizo za mifumo.

9.8 Udhaifu katika usimamizi wa miradi ya TEHAMA

i. Kutokuwepo kwa taarifa na nyaraka za miradi ya TEHAMA. Mwongozo wa usimamizi wa miradi ya TEHAMA wa Serikali Mtandao unahitaji taarifa na nyaraka zote za miradi ziandaliwe katika kila hatua na zihifadhiwe kwa ajili ya mapitio na kuhakikisha taratibu zinafuatwa. Taarifa na nyaraka hizo ni pamoja na nyaraka zinazoelezea; madhumuni na faida za mradi,mpango wa mradi na shughuli zitakazofanywa ikijumuisha kipindi cha utekelezaji,nyaraka zinazoainisha mahitaji ya watumiaji wa mfumo, nyaraka ya usanifu wa mfumo na nyaraka zinazoonesha kufanyika kwa majaribio ya mfumo kama umekidhi mahitaji yaliyoainishwa. Ukaguzi wa miradi miwili ya Maboresho ya Mfumo wa Uhasibu wa Serikali za Mitaa (Epicor) na utengenezaji wa mfumo wa usajili wa makampuni na biashara katika Wakala wa Usajili wa Biashara na Makampuni BRELA, ilibainika kutokuwa na baadhi ya nyaraka tajwa hapo juu kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo.

ii. Udhaifu katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya TEHAMA. Ukaguzi wa usimamizi wa mradi wa kuboresha mfumo wa kihasibu Epicor wa mamlaka za serikali za mitaa na mradi wa utengenezwaji wa mfumo wa kusajili biashara na makampuni katika wakala BRELA ulibaini mapungufu yafuatayo katika usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi.

a) Kwenye mradi wa kuboresha mfumo wa kihasibu (Epicor) katika mamlaka za serikali za mitaa, kunakosekana kumbukumbu za gharama za mradi kadri mradi unavyotekelezwa,. Udhaifu huu husababisha mkandarasi kulipwa

fedha kabla hajamaliza kutekeleza sehemu ya mradi kulingana na mkataba, pia inakuwa ngumu kufahamu gharama kamili ya mradi iliyokwisha kutumika pindi inapohitajika.

b) Mabadiliko yanayoibuliwa na watumiaji wa mfumo baada ya mfumo kukabidhiwa na mkandarasi hayafanyiwi kazi katika kipindi cha uangalizi ambacho mkandarasi huyafanyia kazi hayo mabadiliko pasipo gharama za ziada. Hili lilibainika katika mradi wa kutengeneza mfumo wa Usajili wa Biashara na Makampuni BRELA.

   Hii inaweza kusababisha Taasisi kuingia gharama za kulipia utekelezaji wa hayo mabadiliko.

c) Mapungufu kwenye mafunzo kwa watumiaji wa mifumo baada ya mradi kukamilika na kabla ya mfumo kuanza kutumika. Ili mfumo uweze kutumika ipasavyo na kuleta tija mafunzo kwa watumiaji wa mfumo ni jambo la lazima. Katika ukaguzi wa miradi hii miwili imebainika kukosekana kwa ushahidi wa kuthibitisha kama mafunzo yalifanyika. Pia mafunzo kwa maafisa wa TEHAMA ambao watakuwa na jukumu la kusimamia na kutoa msaada kwa watumiaji hayafanyiki kwa ufanisi kama ambavyo imeanishwa kwenye mkataba na mkandarasi.

d) Mifumo kutofanyiwa majaribio ya kutosha kabla ya kuanza kutumika ili kutambua kama mahitaji yaliyoanishwa na watumiaji wa mfumo yametekelezwa kwenye. Kutofanyika kwa majaribio hupelekea kuwepo kwa mifumo ambayo haikidhi mahitaji ya taasisi na watumiaji.

9.9 Udhaifu kwenye kuhamisha Ujuzi wa kusimamia na kuendesha mifumo.

Utaratibu usiokidhi wa kuhamisha ujuzi kutoka kwa mkandarasi kwenda kwa Maafisa TEHAMA wa Taasisi za serikali. Katika ukaguzi wa utengenezaji wa mfumo wa kusajili biashara na makampuni katika wakala wa usajili BRELA, ilibainika kuwa mkataba ulitaka mkandarasi kuhakikisha kuwa Maafisa TEHAMA wa BRELA wanajengewa uwezo wa kuusimamia mfumo na kuuboresha kwa siku za usoni. Mkataba ulianisha njia ya kuhamisha ujuzi ni kuwashirikisha maafisa TEHAMA kwenye hatua za usanifu na uundwaji wa mfumo jambo ambalo halikufanyika kwa ufasaha kama ilivyokusudiwa.

Hii imesababisha BRELA kuendelea kumtegemea mkandarasi katika kufanya maboresho ya mfumo hivyo kupelekea kuongezeka kwa gharama.

Mapendekezo: Serikali ihakikishe uwepo wa vitengo vya kusimamia miradi ikiwemo ya TEHAMA kwenye taasisi za umma. Aidha, Serikali kupitia wakala wa Serikali mtandao (eGA) kuboresha ufuatiliaji wa usimamizi sahihi wa miradi ya TEHAMA katika taasisi za Serikali. Pia taasisi za serikali kuhakikisha Maafisa TEHAMA wanajengwa uwezo ili kusimamia mifumo baada ya kukabidhiwa mradi na Mkandarasi.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, Mtaa wa Hazina, S.L.P 950,

41104 Dodoma, Tanzania • Simu:+255 (26) 2321759, Nukushi: +255 (26) 2321245

Barua pepe: ocag@nao.go.tz | Tovuti: www.nao.go.tz

www.nao.go.tz